# Uelekeo

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*



## Wafuga nyuki kukusanyika Tz

Uk. 15

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00071 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Juni 26 - Julai 2, 2024 |

## 'Rais wetu anawatambua na kuwajali wajane'

Uk.2


## Mwinyi ataka ushirikiano na Big Win



Uk.3

## Mtambo wa kutibu majitaka kukamilika Oktoba

Uk.3



## `Marufuku CCTV maeneo ya faragha'

Uk.2



### UJENZI HOSPITALI MSOGA:

# JK amshukuru Rais Samia

- Itatoa huduma maeneo ya jirani na abiria wa ajali za barabarani





Uk. 4

# Maandamano Kenya: Hali si shwari

- Wavamia Jengo la Bunge, wanne wadaiwa kupigwa risasi











Uk. 4

## Mambo 6 ya kupunguza msongo wa mawazo unapojiandaa kwa mtihani

Uk. 8

# ‘Samia anawatambua na kuwajali wajane’

**Na Mwandishi Wetu, Songea**

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Rehema Madenge, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anawatambua na kuwajali wajane na kwamba serikali anayoiongoza imetekeleza hatua mbalimbali kuhakikisha changamoto za wajane zinatatuliwa.

Alisema hayo mjini hapa wakati akifungua maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani jana ambayo kimkoa yalifanyika ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Alisema Tanzania kama yalivyo mataifa mengine, inatekeleza mpango wa kijamii kutumia nishati safi ya kupikia ili kuondokana na uharibifu wa mazingira na athari za kiafya.

Kwa mujibu takwimu za Sensa ya Watu na Makazi za mwaka 2022, Mkoa wa Ruvuma una jumla ya wajane 49,702, huku takwimu za kitaifa zikionesha Tanzania ina wajane 1,396,262.

Alisema wajane wengi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali.

“Baadhi ya wajane pia hujikuta wanafukuzwa nyumbani mwao, kutengwa na kunyanyaswa na ndugu wa mume pamoja na jamii na wengine hulazimishwa kuolewa na ndugu wa marehemu pasipo ridhaa yao, pia wengine hukosa utetezi mbele ya vyombo vya sheria wanapotafuta haki zao,” alisema.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Akizungumzia kaulimbiu ya siku ya wajane ya mwaka huu inayosema; Imarisha mifumo ya upatikanaji wa nishati, kukuza uchumi wa wajane na familia, Rehema alisema inasisitiza na kuhimiza matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia.

Mapema risala ya wajane iliipongeza serikali kwa kutambua siku hiyo muhimu ambayo inatoa fursa kwa wajane kutafakari mipango, mikakati, mafanikio na changamoto ili kuimarisha na kuzitatua.

Waliipongeza serikali kwa kutoa fursa ya mikopo inayotokana na asilimia nne ya fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha wanawake wajane kiuchumi ambapo hadi sasa vikundi vitatu vya wanawake wajane katika Manispaa ya Songea vimepatiwa Sh. milioni 5.3.

Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wajane Duniani hufanyika kila mwaka Juni 23 ambapo mwaka huu kwa Mkoa wa Ruvuma, yalifanyika Juni 24.

# ...apongezwa kwa uteuzi unaozingatia jinsia

> Serikali zote mbili, zimetambua uwepo wa wanawake kwa kuwachagua katika sekta mbalimbali ikiwemo mawaziri ambapo sasa kwa Zanzibar wanawake waliopo katika nafasi za maamuzi ni asilimia 33.

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Said Mussa, amempongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa uteuzi anaoufanya kwa kuwa unazingatia jinsia hatua ambayo umeipaisha nchi kwa kuwa na wanawake asilimia 24 katika diplomasia.

Alitoa pongezi hizo wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake katika Diplomasia ambapo kwa mara ya kwanza yaliadhimishwa nchini tangu kuasisiwa kwake na Baraza la Umoja wa Mataifa mwaka 2022.

Alisema Rais Dk. Samia, amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha wanawake wako mbele katika ngazi ya maamuzi kwa kuhakikisha anawachagua katika nafasi mbalimbali.

“Kwa kutambua mchango wa wanawake katika diplomasia, leo hapa tupo na wanadiplomasia nguli kutoka ndani ya nchi na nje, tunaye Balozi Getrude Mongella, Balozi Amina Salum Alli, Balozi Riberata Mulamula na Mabalozi mbalimbali wanaowakilisha nchi zao hapa,” alisema Balozi Mussa.

Kwa upande wake, Waziri wa Maendeleo ya Jamii kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema uwepo wa maadhimisho hayo hapa nchini ni jitihada ya serikali zote za Muungano katika kuhakikisha inamuwezesha mwanamke kuingia katika nyanja zote za maamuzi.

“Serikali zote mbili, zimetambua uwepo wa wanawake kwa kuwachagua katika sekta mbalimbali ikiwemo mawaziri ambapo sasa kwa Zanzibar wanawake waliopo katika nafasi za maamuzi ni asilimia 33,” alisema.

Akizungumzia kuhusu uchumi, Pembe alisema serikali zote zimeweka miundombinu ya kuwainua wanawake ikiwemo kuwapa kipaumbele katika kuwapa mikopo isiyokuwa na riba.

“Wanawake wamepewa kipaumbele kila sehemu kwenye siasa, tunaye Jemedari wetu Rais Dk. Samia, ukienda kwenye uchumi wanawake wapo, kwenye elimu, afya kote serikali imeweka mazingira mazuri kuhakikisha mwanamke anapata nafasi,” alisema.

# ‘Marufuku CCTV maeneo ya faragha’

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), imezionya taasisi na kampuni zinazotumia kamera za usalama maeneo ya kazi (CCTV), kuacha kuweka kamera hizo katika maeneo ya faragha kama vile vyooni.

Aidha, taarifa iliyotolewa na Tume hiyo jijini Dodoma juzi, imetoa wito kwa wadau wote kufanya mapitio ya kina ya vitendo vyao vya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa wanazingatia kikamilifu Sheria na Kanuni za Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

“Heshima kwa faragha ya mhusika wa taarifa ni ya msingi na ni jukumu la kila taasisi kulinda taarifa binafsi za watu,” ilisema.

“PDPC inatoa onyo kali kwa taasisi na kampuni zote zinazotumia kamera za usalama maeneo faragha kuacha kufanya hivyo.

“Taasisi na kampuni zote zinakumbushwa kuzingatia kikamilifu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake wakati wa kufunga mifumo ya usalama maeneo ya kazi au nyumbani,” ilisema.

Taarifa ilisema ni muhimu hatua zozote za ufuatiliaji ziwe za uwiano na zenye kuheshimu haki za faragha za watu.



# Polisi watakaoshiriki mafunzo Nigeria wakabidhiwa Bendera

**Na Abel Paul, Jeshi la Polisi**

POLISI wa kike wanaokwenda Abuja nchini Nigeria kushiriki mafunzo ya askari wa kike Ukanda wa Afrika kuanzia Julai Mosi hadi 9, mwaka huu, wamekabidhiwa rasmi Bendera ya Taifa.

Akiwakabidhi Bendera hiyo Makao Makuu Ndogo ya Jeshi hilo jijini Dar es Salaam juzi, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi nchini, CP Awadh Juma Haji, aliwataka kuzingatia nidhamu wakati wote wa mafunzo yao huko Abuja, Nigeria ambayo yamelenga kuwajengea uwezo.

Alisema miongoni mwa mambo watakayojifunza, ni uongozi, afya ya akili na mengine yanayohusu ulinzi.

Alisema mafunzo hayo yataleta tija kwa Jeshi la Polisi nchini.

Aidha, aliwataka kuzingatia nidhamu ambapo aliwasihi kwenda kwao Nigeria ni kuiwakilisha nchi na italeta sifa kwa nchi na kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Pia aliwataka askari hao kutangaza sifa nzuri ya Tanzania ambayo imeenea duniani kote katika masuala ya amani na utulivu na kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini.



## Tanesco yaanza maboresho ya Luku Kanda za Kusini

**Na Mwandishi Wetu, Rukwa**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limetangaza kuanza rasmi kwa zoezi la maboresho ya mfumo wa Luku kwa mikoa ya Kanda ya Kusini na Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Tanesco, Irene Gowelle, alisema hayo katika ziara ya utoaji wa elimu kwa wateja kupitia vituo mbalimbali vya redio katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Iringa.

Alisema tayari zoezi kama hilo limekwishafanyika mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi, na kwamba kuanzia juzi limeanza rasmi katika mikoa ya Kanda ya Kusini na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Alisema lengo la shirika kufanya maboresho hayo ni kuendana na mabadiliko ya kimfumo na viwango vya mita za Luku vya kimataifa, vilevile kuongeza ufanisi na usalama wa mita za Luku nchini.

# Mwinyi ataka ushirikiano na Big Win mpango wa lishe mashuleni



**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka Taasisi ya Big Win Philanthropy ya Uingereza, kushirikiana na serikali yake kwa mpango wa lishe mashuleni katika kupunguza utoro na kuongeza ufaulu wa watoto.

Alitoa kauli hiyo alipokutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Big Win Philanthropy, Dk. Kesete Admasu na ujumbe wake waliofika Ikulu Zanzibar jana.

Aidha, Dk. Admasu alisema wako tayari kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika fursa za kuwajengea uwezo watendaji wake, viongozi pamoja na ushirikiano wa sekta mbalimbali.

## Mtambo wa kutibu maji taka kukamilika Oktoba

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira mjini Igunga (Iguwasa), inatarajia kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kutibu maji taka ifikapo Oktoba, mwaka huu.

Akitoa taarifa mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Mkurugenzi Mtendaji wa Iguwasa, Mhandisi Humphrey Mwiyombela, alisema ujenzi wa mtambo huo ulianza Julai, mwaka jana na unatarajia kukamilika Oktoba, mwaka huu.

"Pamoja na jukumu la kusambaza maji safi na salama ya kunywa mjini Igunga, Iguwasa tuna jukumu lingine la kuhakikisha mazingira yanakuwa safi," alisema.

Alisema katika kuhakikisha mji wa Igunga unakuwa safi, mamlaka hiyo inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji taka unaogharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.8 fedha kutoka serikalini.

Alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 23 na kukamilika kwake kutawanufaisha jumla ya wakazi 82,768 wa mji wa Igunga na vitongoji vyake.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Igunga, Mafunda Temanya, alisema mradi huo ni muhimu kwa ustawi wa afya za wananchi wa Igunga, hivyo aliwataka Iguwasa kuhakikisha wanamsimamia mkandaraji vizuri ili atekeleze mradi huo kwa wakati.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Igunga, Ebenezer Ole Mainoya, alisema Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasisitiza serikali kupambana na maradhi, hivyo, miradi ya usafi wa mazingira ina mchango mkubwa katika kuboresha afya za wananchi.

# JK amshukuru Rais Dk. Samia

**Na Hellen Mwango**

RAIS Mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, amemshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa ujenzi wa Hospitali ya Msoga ambayo inatoa huduma kwa watu kutoka maeneo jirani na abiria wanaopata ajali barabarani.

Alisema hayo wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Msoga Half Marathon 2024 ambayo ni maalum kwa ajili ya kuchangia afya ya mama na mtoto.

Rais mstaafu Kikwete anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika tukio hilo litakalofanyika Juni 29, mwaka huu kijijini Msoga, Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze.

Alisema pamoja na juhudi za serikali kujenga hospitali hiyo, bado haijakamilika na inahitaji mchango wa jamii kupitia Msoga Half Marathon 2024.

Alisema waandaji wa Msoga Half Marathon 2024, wana mapenzi mema na lengo la kuchangia uboreshaji wa huduma ya mama na mtoto hasa watoto wanaozaliwa kabla ya muda wao.

Alisema lengo la marathon hiyo ni kukusanya Sh. milioni 330 kwa ajili kupigania afya ya mama na mtoto.

Aliwaomba wadau wenye mapenzi mema kujitokeza kwa wingi kutimiza lengo na kuiunga mkono Serikali katika juhudi zake kwenye huduma za afya.

"Serikali inajenga hospitali mpya, imekamilika jengo la wazazi, watoto, upasuaji, X-ray, wodi za wagonjwa baada ya upasuaji na eneo la magonjwa ya mlipuko.

"Bado kuna ujenzi unaendelea wa wodi za wagonjwa wote kwa wanawake na wanaume, tunahitaji wodi ya watoto waliozaliwa kabla ya muda wao kutimia, sipendi wanavyoitwa watoto njiti, nachukia sana, binadamu unamwitaje njiti kwa kweli, Baraza la Kiswahili waangalie jina lingine hili linaniudhi," alisema.

Alisema Hospitali ya Msoga si kwamba inahudumia wakazi wa kijiji hicho pekee, bali wananchi kutoka kona tofauti ikiwamo Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, Ngerengere mkoani Morogoro na abiria wanaopata ajali kutoka mikoa inayotumia barabara ya karibu na hospitali hiyo.

"Bado kuna ujenzi wa wodi za wagonjwa wa magonjwa mbalimbali, nyumba za madaktari na wauguzi unaendelea naishukuru sana serikali na tayari imeanza kutoa huduma hata baadhi ya mashabiki wa Simba majeruhi, walipata huduma katika hospitali hiyo," alisema na kuongeza:

"Chumba cha kuhifadhia maiti tunacho, lakini kina majokofu 12 ambayo hayatoshi, wakati mwingine yanajaa na maiti wanalazwa chini, si vyema kuongelea mambo ya chumba cha maiti, lakini inabidi kwa kuwa tunahitaji jamii ijitokeze kuchangia maboresho na ujenzi zaidi."



Rais Mstaafu Dk. Jakaya Kikwete

"Mimi mwenyewe hapa nikifa, lazima nitapelekwa hapo 'mochwari' kwanza siwezi kuwekwa nyumbani kwangu," alisema kwa msisitizo umuhimu wa jamii kushiriki kuboresha hospitali hiyo.

Alisema huduma zenye mahitaji makubwa, ni za mama na mtoto.

"Niliwahi kwenda pale hospitali nikamkuta mama amejifungua mapacha ambao hawajatimiza muda wa kuzaliwa amewafunga kifuani kwake ni kutokana na kutokuwa na vifaa" alisema na kufafanua:

"Serikali ina mchango wake, lakini jamii pia ina mchango wake, waliobuni Msoga Marathon 2024, nawashukuru sana, walibuni kitu kizuri kwa faida ya Watanzania wote na makadirio yao ni kukusanya Sh. milioni 330 ili kupata mahitaji yote ya msingi wanayotaka kuchangia."

Akizungumzia faida ya hospitali hiyo kwa Watanzania, alisema inasaidia kwa asilimia kubwa kwa kuwa kutoka Kibaha hakuna hospitali nyingine na wote wanahudumiwa Msoga.

"Siku moja basi lililokuwa likitoka jijini Dodoma lilipata ajali, mama alikuwa na mtoto wake anampeleka kwa Mchungaji Mwamposa, mtoto aliumia akalazwa pale kwa matibabu, huwa napita mara kwa mara kuwajulia hali wagonjwa nikaelewa kumbe hospitali hii si ya kuhudumia watu wa Msoga au Chalinze pekee," alisema.

Alisema waandaji wamesema maandalizi yako tayari kwa kuwa wakazi wa Msoga wanajishughulisha na kilimo na ufugaji pamoja na jirani zetu anawaalika Watanzania wenye mapenzi mema kujiunga katika kuchangia harambee hiyo.

Akizungumzia watumishi wa umma kujiandaa kustaafu, Dk. Kikwete alisema alianza kujiandaa akiwa Waziri alinunua eka 20 kwa Sh. 60,000 na aliipandisha hadhi ardhi ya Msoga kutoka Sh. 150,000 kwa heka moja hadi Sh. 300,000 japo wenyeji walipanga bei ndogo alikataa akapandisha hadhi ya ardhi kijijini hapo.

Alisema watumishi wasisubiri wafike miaka 50 ndipo waanze kujiandaa kustaafu, bali wajiandae mapema ili wasipate taabu.

"Nikiwa Waziri, nilikuwa nafuga ng'ombe Bagamoyo, lakini serikali ikalitaka lile eneo kwa ajili ya makazi ya watu, nikaona nirudi kijijini kwetu Msoga, nikanunua eka 20, nikahamishia mifugo yangu, kule Kiwanga nilinunua eka 20 kwa Sh. 60,000, lakini leo hii wapo jirani zangu wanauza eka moja Sh. milioni nane," alisema Dk. Kikwete.

Aidha, alisema ardhi sasa imepanda bei Msoga wapo wajanja walinunua eka moja kwa Sh. 80,000, lakini sasa wanakata vipande wanauza kwa Sh. milioni sita kwa hiyo ujanja kuwahi.

Msoga Marathon inatarajiwa kufanyika Juni 29, mwaka huu kwa ajili ya kuchangia Afya ya Mama na Mtoto.

# Hali si shwari Kenya

**NAIROBI, Kenya**

WATU kadhaa wamepigwa risasi nchini Kenya huku waandamanaji wakiingia katika maeneo ya Bunge la nchi hiyo.

Makumi kwa maelfu ya Wakenya wamekuwa wakiandamana mjini Nairobi tangu asubuhi ya jana, huku maandamano sawia yakifanyika katika miji na majiji mengine kote nchini.

Video kwenye mitandao ya kijamii inaonekana kuonesha maelfu ya watu wakitembea kuelekea Mji Mkuu Nairobi kujiunga na maandamano, ambayo yaliitishwa kupinga msururu wa mapendekezo ya ushuru mpya katika Muswada wa Fedha.

Bunge la nchini Kenya jana lilipitisha marekebisho ya Muswada wa Fedha kwa mwaka 2024.

Muswada huo wa Sheria ya Fedha wenye utata, umepitia Kamati ya Bunge zima ambapo wabunge walikuwa wakipiga kura ya marekebisho ya Muswada huo ambao ulisomwa kwa mara ya tatu,

Hii ni baada ya Wabunge 195 kupiga kura kupitisha muswada huo huku 106 wakipiga kura kukataa sheria iliyopendekezwa.

Makabiliano makali yamezuka katikati ya mji wa Nairobi baada ya polisi kuwatawanya waandamanaji wakipinga Muswada wa Fedha wa 2024. BBC.



# MUHAS kujadili tafiti magonjwa yasiyoambukizwa

**Na Mwandishi Wetu**

CHUO cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), kinatarajia kufanya kongamano lake la 12 la kisayansi litakalojadili tafiti mbalimbali hususan, zenye majibu ya magonjwa yasiyoambukiza.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Appolinary Kamuhabwa, alisemwa hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya kongamano hilo litakalofanyika kwa siku mbili kuanzia Juni 27 na 28, mwaka huu katika Kituo cha Afrika Mashariki cha Umahiri wa Magonjwa ya Moyo, Mishipa na Damu.

Alisema kongamano hilo linatarajiwa kuwa na wajumbe zaidi ya 400 kutoka ndani na nje ya nchi ambapo tafiti za kisayansi 80 zitawasilishwa kwa njia ya maongezi huku nyingine 107 zitawasilishwa kwa njia ya mabango.

Alisema jukumu la MUHAS ni kutoa mafunzo ili kujenga rasilimali kwa watu wa fani ya afya, kufanya utafiti na kushiriki kikamilifu katika utoaji huduma ya afya katika jamii," alisema.

"Kongamano hili ni sehemu ya kumuenzi Mkuu wa kwanza wa Chuo aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili Hayati Ali Hassan Mwinyi. Pia limebeba kauli mbiu isemayo, 'Sayansi kama hadithi ya maisha: nguvu ya tafiti, ubunifu na ushirikiano katika kuimarisha mifumo thabiti wa afya.'

Alisema katika kongamano hilo baadhi ya matokeo ya tafiti zitakazowasilishwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma wodi maalum za kulaza watoto wachanga ni asilimia 48, asilimia 15 ya wagonjwa wa VVU wana kiwango cha juu ya sukari, unywaji wa pombe na shinikio la juu la damu linachangia wagonjwa hawa kuwa na kiwango



**Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Appolinary Kamuhabwa**

cha juu cha sukari.

Alisema tafiti nyingine ni ile iliyofanywa Kinondoni ambapo asilimia 54.5 ya wanawake wanaojichubua wengi wao wanaofanya kazi ya mapokezi.


Alisema kutakuwa na mijadala mingi kuhusu ustawi wa afya ambapo kutakuwa na wataalam kutoka nje na ndani ya nchi.

Mijadala mingine itahusisha ufanisi wa kugharimia mifumo ya afya nchini ambapo watafiti watawasilisha jinsi gani nchi itatekeleza mfumo huu ili kuleta tija kwa wananchi wote, mifumo bora ya kuishi ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.



# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



## Mabosi DAWASA mnajua hili?

Huku uswahilini kwetu kumekuwa na tatizo la mabomba ya maji kutoboka au kukatika mara kwa mara.

Wakati mwingine, ni kutokana na magari au pikipiki lakini ukiwapigia simu watu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) huchelewa sana kufika.

Lakini kuna wale wakata maji mitaani, wanaweza kuja hata mara mbili na kukuta bomba limekatika na kutiririsha maji mtaani lakini hawajali. Yaani wanajali kumkatia mtu maji kwa kushindwa kulipa bili tena miezi miwili tu lakini maji ya DAWASA yanayotiririka hivyo hawajali. Hii haijakaa sawa.




## MAONI YA MHARIRI

# Kuweka kamera mpaka maliwatoni si sahihi

HEBU fikiria unaingia maliwatoni kujisaidia, ukiwa hujui hili wala lile, kumbe kila unachofanya humo watu wanakuona au kama wavyosema vijana wa vijiweni, 'watu wanakupiga chabo'!

Heri iishie kukipiga chabo kwa jicho na jambo likaisha siku hiyo lakini hapa taswira yako inarekodiwa na mtu au watu wakitaka kukuona tena na tena muda wowote ulivyokuwa 'ukijinafasi' wanakuona!

Ni katika muktadha huo, jana, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), ilizionya taasisi na kampuni zinazotumia kamera za usalama maeneo ya kazi (CCTV), kuacha kuweka kamera hizo katika maeneo ya faragha kama vile vyooni.

Tume hiyo imetoa wito kwa wadau wote kufanya mapitio ya kina ya vitendo vyao vya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa wanazingatia kikamilifu Sheria na Kanuni za Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Tume imekumbusha kwamba heshima ya mtu kwa faragha yake ni ya msingi na ni jukumu la kila taasisi kulinda taarifa binafsi za watu. Tume ikatoa onyo kali kwa taasisi na kampuni zote zinazotumia kamera za usalama maeneo ya faragha kuacha kufanya hivyo.

Tume imesisitiza umuhimu wa taasisi kuzingatia kikamilifu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake wakati wa kufunga mifumo ya usalama maeneo ya kazi au nyumbani.

Ingawa tunaamini kama zipo taasisi zinazoweka kamera hadi maeneo ya faragha ni chache, tunaunga mkono kwa dhati kabisa hatua hii ya PDPC na hivyo kama zipo zinazofanya hivyo ziondoe mara moja hizo kamera. Na Waswahili wanasema lisemwalo lipo, kama halipo laja.

Na kimsingi, mtu yeyote mwenye akili timamu akigundua kwamba huko maliwatoni kumbe hana faragha yoyote, hata haja yake, iwe ndogo kubwa inakata palepale!

Ingawa Tume umejielekeza kwa taasisi lakini huenda kuna watu binafsi na wamiliki wa sehemu za mikusanyiko ya watu wengi kama kwenye mabaa na mahoteli wamefunga pia kamera za ulinzi hadi maeneo haya faragha.

Wanaweza kuwa wamefunga kwa ajili ya ulinzi lakini kufunga kamera hadi vyooni haikubaliki abadani.

Tunaamini kwamba onyo hili pia linawahusu watu binafsi kwani Sheria na Kanuni za Ulinzi wa Taarifa Binafsi hazibagui na hivyo kama wapo waondoe mara moja hizo kamera au hatua kali zichukuliwe juu yao.

## Wasiliana nasi


| | |
|---|---|
| **Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000 | **S. L. P:** 15110, Dar es Salaam |
| **Mhariri wa Habari:** +255768411003 | **Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro |
| **Mhariri Michezo:** +255784122020 | **Jengo la:** Aura Mall |
| **Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825 | **Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532 |
| | **Email:** uelekeohabari@gmail.com |


Na Hamid Yassin

## JICHO LANGU

# Elimu uchaguzi Serikali za Mitaa itolewe mapema

TANGU kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchi ni miaka 32 iliyopita (Juni, 1992), Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu utakuwa wa 11 na umepangwa kufanyika mwezi Novemba.

Naweza kusema uchaguzi huo ulikuwa ukifanyika kwa usawa japokuwa manung'uniko ya hapa na pale hayakosekani ikizingatiwa nafasi hizo hugombaniwa na vyama tofauti vya siasa.

Mpigakura katika uchaguzi wa serikali za mitaa ni mtu yeyote ambaye ni raia wa Tanzania aliyefikisha umri wa miaka 18 na kuendelea, anaweza kuwa mkazi anayeishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Mtaa kwa upande wa mijini au anaishi kwenye eneo la kijiji au mitongoji na ambaye ama ana kaya au anaishi katika kaya au yaasisi iliyopo katika eneo hilo.

Mpigakura lazima majina yake yawemo kwenye orodha ya wapigakura na kwamba Msimamizi Msaidizi atajiridhisha juu ya uhalali wa mpigakura ambako huko miaka ya nyuma alitakiwa kuonesha moja kati ya 'utitiri' wa vitambulisho vifuatavyo vikiwemo cha mpigakura, cha kazi, hati ya kusafiria (passport) na kadhalika.

Lakini kuanzia uchaguzi wa mwaka 2019 vimekuwa vikitumika vitambulisho viwili tu, cha mpigakura na kile cha Taifa, yaani cha NIDA. Cha taifa kilitumika kama mwananchi hakuwa na kile cha mpigakura.

Pia huwa kuna utaratibu wa kupiga kura na mahitaji mengine muhimu, kama vile atatokea mpiga kura ambaye ana ulemavu wa macho au ulemavu wowote wa kimaumbile au hajui kusoma na kuandika, anaweza kumuomba mtu aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura.

> **Mpigakura lazima majina yake yawemo kwenye orodha ya wapigakura na kwamba Msimamizi Msaidizi atajiridhisha juu ya uhalali wa mpigakura ambako huko miaka ya nyuma alitakiwa kuonesha moja kati ya 'utitiri' wa vitambulisho vifuatavyo vikiwemo cha mpigakura, cha kazi, hati ya kusafiria (passport) na kadhalika.**

Isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Mgombea au mwakilishi wake.

Pia huwa kuna marufuku kadhaa ikiwemo kuharibu orodha ya wapiga kura, mgombea kutoa taarifa za uongo, kuharibu karatasi za wagombea, kughushi karatasi za uteuzi, kupiga kura zaidi ya moja.

Vingine ni kuvuruga kwa kutishia wapigakura au wagombea, kufanya kampeni siku ya uchaguzi, kuvaa mavazi au nembo za chama, kumzuia msimamizi wa uchaguzi kufanya kazi yake, kukiuka masharti ya kiapo chake, kukiuka kanuni na kupatikana na karatasi zaidi ya moja za mgombea mmoja.

Masuala haya na kama kuna mengine mapya huu ndiyo wakati wake kwa watakaosimamia uchaguzi kutoa elimu ya uchaguzi huo wa Serikali za mitaa badala ya kusubiri hadi dakika za mwisho ndipo wahusika wakurupuke kuelimisha

# Hatua muhimu za kufikia malengo ya mauzo



**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA ulimwengu wa biashara, mafanikio hayaji kwa bahati nasibu bali huhitaji mipango makini, juhudi endelevu na zaidi ya yote, malengo yanayopimika.

Kama ilivyo katika shughuli yoyote ya kiuchumi au kijamii, lazima kuwe na malanego.

Na vivyo hivyo, kwenye tasnia ya mauzo, malengo ni sehemu muhimu mno ya kufanikisha faida kupitia ongozeko la mauzo.

Kuweka malengo ya mauzo, ni mojawapo ya nyenzo muhimu kwa biashara yoyote inayolenga ukuaji na ustawi.

Chukua fursa hii kabla ya kuendelea kusoma makala kwa kujiuliza swali hili. Je; una malengo ya mauzo kwenye biashara yako?. Kama jibu ni ndiyo, vyema. Na kama jibu ni hapana, tambua hauko makini na biashra yako.

Hivyo basi, anza sasa kutengeneza mipango ya kukuwezesha kuanza kuweka malengo ya mauzo. Malengo haya yakiwepo, ni rahisi kujua kule biashara yako inakoelekea. Kama kuna dalili za kufifia au kisinyaa kwa soko, itakusaidia kujipanga na kujilinda na hasara.

Malengo haya yanatoa mwongozo na dira kwa timu ya mauzo, huku yakiwawezesha kufuatilia na kuboresha utendaji wao.

Katika makala haya, tutachunguza umuhimu wa kuweka malengo ya mauzo, njia bora za kuyafikia na jinsi ya kuhakikisha kikosi kazi chako cha mauzo, kinabaki kwenye mstari sahihi wa mafanikio.

### UMUHIMU WA KUWEKA MALENGO YA MAUZO

Malengo ya mauzo ni muhimu kwa sababu kadhaa. Kwanza, yanaweka matarajio wazi kwa timu yako. Bila malengo, timu ya mauzo inaweza kukosa mwelekeo, hali itakayopunguza ufanisi wao. Malengo yanatoa kipimo cha utendaji na hivyo kuruhusu timu na uongozi kutathmini maendeleo na kufanya marekebisho inapohitajika. Zaidi ya hayo, malengo yanawapa wafanyakazi motisha.

Malengo yanapowekwa vizuri, yanakuwa kama changamoto inayowafanya wafanyakazi wajitahidi zaidi ili kuyafikia na hata kuyapita.

Kama vile tunayoweka malengo kwenye maisha, ndivyo tunavyohitajika kuwa na malengo katika idara ya mauzo kwenye biashara zetu. Kama bado huna malengo ya mauzo,

tafuta mtu mzoefu wa kukusaidia kuweka msingi imara wa kuweka malengo sahihi ya mauzo.

### MBINU BORA ZA KUWEKA MALENGO YA MAUZO

Malengo Mahususi na anayopimika.

Ni muhimu kuhakikisha malengo yako ni mahususi na yanayopimika. Badala ya kusema `tunahitaji kuongeza mauzo,' sema `tunahitaji kuongeza mauzo kwa asilimia 20 ndani ya miezi sita ijayo.'

Malengo haya yanaweka viwango vya wazi vya mafanikio na kuruhusu timu kufuatilia maendeleo kwa urahisi.

### MALENGO YANAYOWEZA KUFIKIWA NA YANAYOFAA

Weka malengo yanayoweza kufikiwa, lakini pia yanayotoa changamoto. Malengo yanayoweza kufikiwa yanahakikisha

timu haikati tamaa mapema, wakati malengo yanayotoa changamoto yanahakikisha kuwa timu inafanya juhudi za ziada.

Kwa mfano, ikiwa timu yako imekuwa ikiongeza mauzo kwa asilimia 10 kila mwaka, jaribu kuweka lengo la asilimia 15 au 20. Hii itachochea ubunifu na jitihada za ziada.

### MALENGO YANAYOENDANA NA MUDA

Malengo yanapaswa kuwa na muda maalum wa kuyafikia. Hii inaweka hali ya dharura na kuzuia uzembe. Weka muda unaofaa ambao unatoa nafasi ya kutosha kufikia lengo, lakini pia unahakikisha kuwa timu inaendelea kujitahidi.

Kwa mfano, lengo la kuongeza mauzo kwa asilimia 20 ndani ya mwaka mmoja, linaweza kuwa na hatua ndogo ndogo za kila robo mwaka ili kufuatilia maendeleo.

### HATUA MUHIMU ZA KUFIKIA MALENGO YA MAUZO

Tafiti na uchambuzi wa soko:

Kabla ya kuweka malengo, ni muhimu kufanya utafiti wa kina wa soko. Fahamu mwenendo wa soko, tabia za wateja na ushindani.

Hii itakusaidia kuweka malengo yanayoendana na hali halisi ya soko na kuepuka kuweka malengo yasiyo halisi.

#### Jenga mkakati wa mauzo:

Baada ya kufanya utafiti wa soko, jenga mkakati wa mauzo unaoendana na malengo yako. Mkakati huu unapaswa kujumuisha njia za

kuvutia wateja wapya, kuhifadhi wateja wa zamani, na kuongeza thamani ya mauzo kwa kila mteja.

Kwa mfano, unaweza kuanzisha programu za uaminifu au ofa maalum za msimu.

#### Mafunzo na maendeleo ya timu:

Hakikisha timu yako ina vifaa na ujuzi wa kutosha kufikia malengo. Wekeza katika mafunzo na maendeleo ya timu. Mafunzo ya mara kwa mara kuhusu mbinu mpya za mauzo, matumizi ya teknolojia, na huduma kwa wateja yanaweza kuongeza ufanisi wa timu.

#### Teknolojia na zana za kisasa:

Tumia teknolojia na zana za kisasa kusaidia timu yako kufikia malengo. Programu za usimamizi wa mahusiano na wateja (UMW) maarufu kama UMW, uchambuzi wa data na zana za mawasiliano zinaweza kurahisisha kazi na kuongeza tija. Kwa mfano, mfumo wa UMW unaweza kusaidia kufuatilia wateja na mauzo kwa urahisi, huku ukitoa taarifa muhimu kwa wakati halisi.

#### Motisha na zawadi:

Tia motisha timu yako kwa kutumia mfumo wa zawadi. Hiiinaweza kuwa katika mfumo wa bonasi, likizo za ziada au kutambua na kusherehekea mafanikio yao.

Motisha zinaweza kuongeza ari ya kufanya kazi na kuhakikisha kila mtu anafanya kazi kwa bidii ili kufikia malengo.

#### KUFUATA NA KUREKEBISHA.

Malengo:

Ni muhimu kufuatilia maendeleo ya malengo kwa wakati halisi. Hii inasaidia kugundua changamoto mapema na kufanya marekebisho inapohitajika. Tumia ripoti za mara kwa mara, mikutano ya tathmini, na maoni kutoka kwa timu yako ili kuhakikisha kuwa mko kwenye njia sahihi.

Kama sehemu ya utaratibu huu, kuwa tayari kubadilisha malengo yako inapohitajika.

Soko linaweza kubadilika, na hivyo, malengo yako yanapaswa kuwa ya kubadilika pia.

Kwa mfano, ikiwa kuna mabadiliko makubwa katika uchumi au ushindani, unaweza kuhitaji kurekebisha malengo yako ili kuendana na hali mpya.

Ni muhimu kukumbuka kuwa kuweka malengo ya mauzo ni sanaa na sayansi inayohitaji utafiti, mipango, na utekelezaji makini. Malengo haya yanatoa mwelekeo, motisha, na kipimo cha mafanikio kwa timu ya mauzo.

Kwa kutumia mbinu bora za kuweka malengo, kuchukua hatua sahihi za kuyafikia, na kufuatilia maendeleo kwa karibu, biashara yoyote inaweza kujiweka kwenye njia ya mafanikio makubwa. Kama msemo wa Kiswahili unavyosema, `lengo halitimii bila bidii,' na hivyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa timu yako inafanya kazi kwa bidii na kwa mwelekeo sahihi ili kufikia malengo ya mauzo na kustawi katika soko lenye ushindani.

# Mambo 6 ya kupunguza msongo wa mawazo unapojiandaa kwa mtihani



UNAPOSOMA kwa ajili ya mtihani, unaweza kuhisi msongo wa mawazo na kuelemewa na maandalizi yako ya mtihani.

Mfadhaiko ni sehemu ya kawaida ya maisha ya mwanadamu na mtihani unaweza kukupa wakati mgumu sana.

Hata hivyo, kuna njia za kudhibiti msongo wa mawazo na kudumisha ustawi wako.

Kujiwekea tabia nzuri za kudhibiti mfadhaiko, kutachangia ustawi wako wa kisaikolojia na hatimaye utendaji wako katika masomo.

**. PUMUA**

Kitu cha kwanza cha kufanya unapohisi msongo wa mawazo, ni kupumua kwa nguvu.

Unapoanza kuhisi mfadhaiko, mapigo ya moyo huongezeka, viganja hutokwa na jasho na shinikizo la damu huongezeka.

Ukivuta pumzi kidogo wakati hisia hii inapoanza, unaweza kudhibiti mapigo ya moyo na kupunguza mfadhaiko mwilini.

Baada ya kupumua, kuna mambo mengine unaweza kufanya ili kujisikia vizuri.

**. WEKA MALENGO YANAYOWEZEKANA**

Ni muhimu sana kuweka malengo yanayowezekana ambayo unaamini utayafikia.

Usiweke vitu vingi kwenye orodha yako ya mambo ya kufanya - hili litakufanya utakuwa na wasiwasi. Fikiria juu ya kile kinachowezekana kwa wakati ulio nao, na uweke malengo ya maendeleo endelevu.

Kumbuka kupanga muda wa kujiliwaza mwenyewe na usisahau kujipongeza kwa mafanikio yako.

**. CHUKUA MAPUMZIKO**

Hakuna mtu anayeweza kufanya kazi moja milele, kama vile kusoma tu siku nzima. Baada ya muda, utachoka na hutaweza kukamilisha kazi zako.

Inaweza pia kumaanisha utahitaji nguvu zaidi ili kukamilisha kazi fulani katika kiwango chetu cha kawaida na kusoma kwa muda mrefu kunaongeza hatari ya kufanya makosa.

Kwa hivyo, kuchukua mapumziko kutaboresha uwezo wako wa kusoma. Ikiwa unaona umetumia muda mrefu kusoma, acha na fanya jambo lingine.

**. TOKA NJE YA NYUMBA YAKO**

Shughuli ya kimwili ni muhimu sana kuboresha afya yako na kupunguza msongo. Mfano; kutembea, kukimbia au kucheza mchezo unaopenda.

Hii itaifanya akili yako iache kuwaza masomo muda wote na utawaza mambo mengine unayoyaona huko nje. Na mazoezi siku zote ni kitu kizuri kwa ajili ya afya ya mwanadamu.





**. TAFUTA MARAFIKI**

Maingiliano ya kijamii, ni chanzo muhimu cha ustawi kwa vijana.

Unaweza kuzungumza na marafiki mtandaoni, lakini matumizi makubwa ya mitandao ya kijamii yanaweza pia kuwa na athari mbaya kwa ustawi.

Ni muhimu kudumisha uhusiano wa nje ya mtandao; panga kukutana na marafiki zako kabla ya mtihani na ufurahie wakati huo pamoja nao.

Mapumziko baada ya masomo ni fursa nzuri ya kubadili mawazo.

Kwa nini usikutane na rafiki kwa matembezi kwenye bustani au kwenye barabara?

**. FANYA MAAMUZI YENYE AFYA**

Unywaji wa vinywaji vya vikali unaweza kusababisha utendaji duni katika masomo, kama vile unywaji wa pombe au utumiaji wa sigara.

Badala ya kunywa kinywaji cha kuongeza nguvu, kunywa tu maji au chagua chakula chenye lishe, kama vile matunda.

Na badala ya kuchelewa kulala, upe kipau mbele usingizi wako.

Kukatiza usingizi kunaweza kuvuruga hisia zetu na kinyume chake, kupata saa za kutosha za kulala ni jambo bora kwa afya.

Mchanganyiko wa tabia zenye afya na shughuli unazopenda ni kichocheo cha kufaulu katika mitihani na udhibiti wa mafadhaiko.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo

JARIDA

# Jungu Kuu

| Jumatano Juni 26 - Julai 2, 2024 |




Jarida hili haliuzwi

# Serikali ifanyie kazi hoja chanya Bajeti 24/25

UK. 12 & 13





# Kutunza mazingira liwe suala la kufa na kupona

**Na Dkt. Felician Kilahama**

Namshukuru Mungu Mwenyezi kwa kuwa ndiye anayetujalia kupumua, uhai na afya njema. Watu wote walioumbwa kwa sura na mfano wake Mungu, hatuna budi kumtolea Mungu shukrani za dhati kwa maana ndiye mwingi wa rehema na fadhili zake kwetu ni za milele.

Makala haya yamejikita kwenye taswira ya uhifadhi wa mazingira katika makazi yetu na kuhimiza kufanyia kazi msemo huu maridhawa kwamba 'Yatunze mazingira ili nayo yakutunze.'

Eneo la Tanzania Bara (Tanganyika) lina miaka 63 tangu liwe huru baada ya kutawaliwa na Waingereza tangu 1918 hadi Desemba 9, 1961. Vilevile, ni miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kuanzishwa kutokana na Tanganyika kuungana na Zanzibar, Aprili 26, 1964.

**WATU, MIFUGO INAONGEZEKA**

Pamoja na idadi ya watu, mifugo na wanyamapori kuongezeka kila mwaka, eneo la ardhi linabaki lilelile au wakati mwingine kupungua. Uzoefu unaonyesha kuwa chanzo kikubwa cha kupungua ardhi inayotegemewa kwa kilimo/ufugaji ni mimomonyoko ya udongo au kumeguka ardhi kutokana na kasi kubwa ya maji ya mvua kwenye eneo lililoachwa wazi kupitia shughuli mbalimbali za kibinadamu zisizokuwa endelevu.

Pia bahari imekuwa ikitanuka na kula eneo la nchi kavu taratibu kutokana na ongezeko la maji linasababishwa na hali nyingi ikiwemo ya ongezeko la joto linaloyeyusha theluji katika baadhi ya maeneo ya dunia na kimsingi maji yakipata joto hutanuka.

**MISITU, ARDHI YA KILIMO VINAPUNGUA**

Kulingana na takwimu za Juni 14, 2024 zinazotolewa na Umoja wa Mataifa (United Nations) kupitia mifumo yake wa kidijiti, mathalani, "Worldometer"; kiwango cha kutoweka misitu (forest-loss) kidunia iimefikia hekta (ha) 2.4 milioni kwa mwaka. Kadhalika, kiwango cha kupotea ardhi (land-loss) kutokana na sababu mbalimbali za kibinadamu pia kimefikia hekta 3.2 milioni.

Tanzania Bara, tunakabiliwa na changamoto hizo: kutoweka misitu asilia kwa kiwango cha hekta 372,000 kwa mwaka lakini pia tishio la kupoteza ardhi inayofaa kwa kilimo kutokana na mmomonyoko wa udongo au kumeguka ardhi sehemu mbalimbali nchini hasa kwenye miteremko mikali ambako kanuni za kilimo-hifadhi zimekuwa hazizingatiwi.

**YALIYOPITA YANAFURAHISHA**

Wakati tunapata uhuru mwaka 1961, hali ya vijito (streams) mito (rivers) kwenye mikoa yote ilikuwa nzuri. Kingo zake tangu kijito au mto ulipoanzia hadi mwisho unapoingiza maji baharini, ziwani au bwawani; zilikuwa zimefunikwa na uotoasili (misitu, aina nyingine za mimea pamoja na nyasi).

Kadhalika, vina vyake (river beds) vilikuwa chini kulingana na ikolojia ya mahali husika. Mathalani kwa wale wanaokumbuka hali ilivyokuwa kwa Mto Msimbazi katika miaka ya 1970: maji yalikuwa yanatiririka vizuri yakiwa safi bila ya taka ngumu au kusheheni udongo, mchanga na matope kama ilivyo nyakati hizi hadi kupelekea kutengeneza vilima ambavyo havikutarajiwa kuwepo kandokando ya kingo za mto.

Miaka ya 1950 hadi 1980, mvua zilikuwa zinanyesha kwa wakati na nyingi hadi mito kusheheni maji mengi lakini ilikuwa mara chache sana kutokea madhara hatarishi kama ilivyo sasa.

Nakumbuka mwaka 1969 nikisafiri wakati wa likizo kuelekea nyumbani wakati wa masika, tulipofika mkoani Singida tulikuta mto umefurika maji na magari hayakuweza kupita ila abiria tukavuka kwa miguu na kupanda gari ililokuwa mbele na waliokuwa kwenye gari hilo wakapanda tuliloliacha nyuma.

Vilevile, kwa mara ya kwanza nilipofika katika Manispaa ya Moshi 1974; nikiwa hapo Moshi nilikuwa nasikia sauti/maporomoko kutokana na maji yaliyokuwa yakibubujika kwenye mito yakielekea uwanda wa chini bondeni.

Kadhalika, ilikuwa vigumu kuona kilele cha Mlima Kilimanjaro kutokana na mawingu mazito juu yake. Mkibahatika kuona kilele hali yake ilikuwa ya kupendeza sana kutokana na sehemu kubwa kusheheni theluji/barafu wakati huohuo misitu ikiwa imeshikamana vizuri kwa kuuzunguka mlima wote.

Miaka ya 1970, wakati nikisomea shahada ya kwanza; Kitivo cha Kilimo, Kampasi ya Morogoro, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM); Milima ya Uluguru ilikuwa inafunikwa na mawingu mazito hadi kwenye eneo lililokuwa ni tovuti ya asubuhi (morning site). Vilevile kulikuwepo na vijito vinavyotiririsha maji mwaka mzima.

Kwa miaka mitatu niliyokaa Morogoro (1974 hadi 1977) sikuwahi kushuhudia matukio ya mioto kwenye misituasili kama ilivyokuja kuwa kwa miongo mitatu iliyopita. Kwa ujumla miaka hiyo, Tanzania Bara, katika ujumla wake, hali ilikuwa ni kijani zaidi maana nchi nzima ilifunikwa na uotoasili ikiwemo misitu mikubwa, mbuga zilizosheheni aina mbalimbali za mimea/nyasi pamoja na ardhioevu ya kutosha kuhifadhi maji ya mvua kwa muda mrefu. Wakati huo, mito ilikuwa na maji ya kutosheleza karibu majira yote hata wakati wa kiangazi hayakukosekana.

**HALI SASA SI HALI**

Nyakati hizi, hali kama hiyo imebaki historia kutokana na shughuli nyingi za kibinadamu zisizokuwa endelevu hadi kupelekea uotoasili kutoweka kwa kasi kubwa na kusababisha kushamiri kwa mmomonyoko wa udongo, mchanga na matope mpaka kumeguka ardhi. Matokeo ya hali hii ni udongo mzuri kusafirishwa na kasi kubwa ya maji inaponyesha mvua kubwa na kuikuta ardhi iko tupu bila kufunikwa na uotoasilia.

Katika hali hiyo mito husafirisha udongo, mchanga na matope pamoja na takangumu hadi baharini; kwenye maziwa na katika mabwawa hivyo, kupunguza vina vyake kwa kiasi kikubwa.

*Inaendelea uk. 18*

# Ziara Chadema Kaskazini zinavyompaisha Dk. Samia

**Na Hamid Yassin**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kinafanya mikutano ya hadhara katika mikoa minne ya Kanda ya Kaskazini katika kile wanachodai ni Operesheni yake ya kukijenga chama chao, lakini kinyume chake sasa wanamnadi vema Rais Dk. Samia Suluhu Hassani kwani hakauki midomoni mwao!

Akitangaza ziara hiyo ya Chadema, Katibu wa Chama hicho Kanda ya Kaskazini, Amani Golugwa alisema mikutano hiyo itafanyika katika mikoa minne ambayo ni Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro.

Golugwa alisema kuwa, operesheni hiyo ya siku 21 itafanyika katika majimbo 35 yaliyopo kwenye mikoa hiyo na itaongozwa na Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe.

Amesema katika majimbo ya Ngorongoro na Karatu kutafanyika mikutano mitano kila jimbo na itaongozwa na Mwenyekiti Mbowe na Makamu Mwenyekiti wa Taifa, Tundu Lissu.

"Kwa majimbo ya Ngorongoro na Karatu tunatarajia kufanya mikutano mitano katika majimbo hayo, na kwa upekee Mwenyekiti wa Taifa atashirikiana na Makamu Mwenyekiti Lissu," amesema.

**AJENDA DHAIFU**

Baada ya kufuatilia hotuba za viongozi wa chama hicho katika maeneo ambayo wameshapita, nimebaini hakuna ajenda ya kuimarisha Chadema wala kukijenga zaidi ya kutumika kuwaonyesha umma wa Watanzania kwamba ndani ya chama hicho hakuna ugomvi wala misuguano miongoni mwa viongozi wao!

"Tunataka kuonyesha CCM na wapinzani wetu wengine na Watanzania kwa ujumla kwamba tuna watu, tuna Mungu, tuna nguvu. Hiyo ndiyo fahari yetu na uimara wetu Kanda ya Kaskazini ambayo ni ngome ya Chadema," aliongea Mbowe.

Mwenyekiti huyo wa Chadema huku akiwa na Makamu wake Tundu Lissu anamuuliza Dk. Samia; "Haya kiko wapi si ulisema hatuelewani? Mbowe hana ugomvi na Lissu wala kiongozi yeyote wa Chadema, mimi ni Baba wa Wana- Chadema wote, sina upande, leo nipo hapa na Lissu aibu iko kwako na wapinzani wetu wengine," aliongea kwenye mkutano wao hadhara kule Karatu.

Hivi tangu Chadema waanze kulumbana wenyewe kwa wenyewe, Rais Dk. Samia ameshawahi kutoa neno lolote juu ya sitofahamu ndani ya chama hicho? Jibu ni hapana.

Binafsi sijamsikia Rais siyo kugusia tu bali hata kutamka neno juu ya 'songombingo' iliyozuka ndani ya chama hicho katika kipindi hiki cha chaguzi zao za ndani. Hivi kumsingizia au kumlisha maneno ya ovyo ambayo Dk. Samia hawajawahi kuongea ndiyo kuijenga Chadema na kuimarisha? Kama ndivyo basi imekula kwao; hapo wanachofanya ni kumnadi yeye vema kwenye mikutano badala ya kuimarisha chama chao!

Katika mikutano inayoendelea ya Chadema pia inazungumzia ushiriki wao kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye mwaka huu huku wakitamba kufanya vizuri eti kama mizengwe haitakuwepo!

**WATU WASAHAULIFU**

Chadema hawaeleweki na wepesi sana kusahau, si hivi karibuni tu hapa walidai hawatashiriki uchaguzi wowote bila kupatikana Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi?

Sasa hizi kampeni zisizo rasmi wanazofanya kwenye mikutano yao huko Kaskazini ya Tanzania kutaka kushinda uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na ule Uchaguzi Mkuu mwakani zinatoka wapi?

Ama tayari Katiba Mpya na Tume Huru wanazotaka wao zimeshapatikana? Waache mazingaombwe ya kisiasa, Hivi sasa Watanzania wanaona kila kinachofanyika ndani ya taifa hili chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Dk. Samia.

**KAULI YA LOWASSA**

Wanataka kushinda chaguzi mbele ya CCM, wamejipanga? Hebu wakumbuke kauli ya aliyekuwa mgombea wao wa urais mwaka 2015 hayati Edward Lowassa, halafu wakae chini wajitafakari!

Nakumbuka maneno ya aliyekuwa mgombea wa Chadema, marehemu Edward Ngoyayi Lowassa kwenye kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 25 mwaka 2015 kuwa, wapinzani kama hawakushinda uchaguzi mkuu mwaka ule, basi wategemee kufanya hivyo baada ya miaka hamsini ijayo.

Hadi hivi karibuni, sikuwa naamini kwamba, marehemu Lowassa alimaanisha katika kauli yake ile zaidi ya kuwa lugha za kuwatahadharisha wapigakura wasifanye 'makosa' ya kumchagua aliyekuwa mgombea wa CCM hayati Dk. John Pombe Magufuli.

Kama kweli Lowassa alimaanisha katika kauli yake ile, basi hakuna haja ya kuwa na vyama vya upinzani kama Chadema katika medani ya siasa za hapa nchini, kwani miaka hamsini (nusu karne) kutoka wakati ule ni kipindi kirefu sana.

Sasa hivi Chadema inafanya kazi ipi iwapo wanaamini wangeshindwa kutumia fursa ya kuiondoa CCM mwaka ule madarakani basi hawataweza kuiondoa madarakani CCM kamwe katika kipindi hicho cha miaka 50.

Wahenga walinena; "Ulimi uliponza kichwa" na pia wanasema "ulimi huumba". Hata kama Lowassa alikuwa anapiga propaganda ili atimize ndoto yake ya muda mrefu ya kuingia Ikulu kupitia mgongo halali wa wapigakura, sasa imekula kwao na wasubiri hiyo 'miaka hamsini' ipite ili wajaribu tena bahati yao.

Na kwa kauli wanazozitoa hivi sasa viongozi wa Chadema, ni dhahiri shahiri kuwa, wameshakata tamaa ya kufanya mipango ya kuing'oa CCM madarakani katika miaka ya hivi karibuni.

Na wanachofanya kule Kanda ya Kaskazini katika ziara yao hii ya siku 21 ni kutumia muda mrefu kuikosoa CCM na viongozi wake wakati wenyewe walishatamka hawana ubavu wa kuingia Ikulu, mi naona ni ziara ya kukipigia debe Chama tawala kwa mlango wa uwani!

**HAWANA SERA MBADALA?**

Tuliosoma Cuba huwa tunategemea kusikia sera mbadala. Kwa mfano, sasa hivi tuna elimu bila malipo na kwa upande wa vyuo vikuu kuna mikopo. Yote haya yanamhakikishia mtoto wa maskini kusoma ngazi zote za elimu bila shida.

*Inaendelea uk. 18*



# Serikali ifanyie kazi hoja chanya Bajeti 2024/2025



**Na Hamisi Kibari**

Tangu Bajeti Kuu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipowasilishwa bungeni Juni 13, 2024 na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, wabunge walipata muda wa kuisoma na kisha kuanza kuijadili.

Sambamba na Bajeti, wabunge wamekuwa pia wakijadili Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25 uliowasilishwa na Waziri katika Ofisi ya Rais anayeshughulikia Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo.

Kama kumbukumbu zangu ni sahihi, leo mjadala utakamilika na hivyo wabunge wanatarajia kupiga kura kuikubali au kukataa Bajeti hiyo ya serikali. Lakini kumbuka kama wabunge wataipigia kura ya 'hapana' kwa asilimia kubwa, jambo ambalo halitegemewi kutokea, Rais Samia Suluhu Hassan atalazimika kulivunja Bunge.

Yapo mengi yamejadiliwa bungeni na hata nje ya Bunge ambayo ninaamini yamemfikia pia Waziri Dkt. Nchemba na ambayo bila shaka serikali yetu sikivu haitaacha kuyatilia maanani.

Baadhi ya hoja nilizopanga kuzigusia katika makala haya ni zinazohusu kupunguza matumizi ya pesa taslimu (kwenda cashless economy); ubadhirifu na umuhimu wa ubanaji wa matumizi; mbinu za kusimamia upungufu wa sukari; suala gesi inayotumika kwenye magari, kikokotoo na adhabu kwa mfanyabiashara kutokutoa risiti.

### MATUMIZI YA FEDHA TASLIMU

Wabunge wanaona moja ya changamoto katika kukusanya kodi ni matumizi makubwa ya fedha taslimu huku serikali ikishindwa kufuatilia miamala ya biashara kwa sababu ya malipo kufanyika kwa pesa taslimu.

Ni kwa msingi huo, wabunge wanapendekeza Sheria ya Mifumo ya Malipo Sura 437 na Sheria ya Usimamizi wa Kodi sura ya 438 ziangaliwe upya kwa kuanzisha sharti la kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa.

Ninachokumbuka Waziri Mwigulu siku moja aligusia hili akisema hilo ni jambo ambalo serikali inalifanyia kazi na hasa inalenga kuongeza matumizi ya lipa kwa namba.

Matumaini yangu ni kwamba wakati wa majumuisho Waziri atatoa ufafanuzi zaidi kuhusu hili na kuharakisha matumizi ya cashless economy na hasa kwa kuzingatia kwamba matumizi ya simu za mikononi na intaneti yamekuwa yakiongezeka.

Itakumbukwa kwamba Mei 16, 2024 Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nape Nnauye, wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Bungeni alisema kwamba laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 62.3 Mwezi Aprili, 2023 hadi kufikia laini milioni 72.5 Mwezi Aprili, 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.4.

Nape pia alisema watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka milioni 33.1 Mwezi Aprili, 2023 hadi kufikia milioni 36.8 Mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 11.2.

Alibainisha kwamba katika kipindi hicho, pia watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya mtandao wa simu waliongezeka kutoka milioni 44.3 hadi kufikia milioni 53.0 mwezi Aprili, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 19.6.

Aidha, Waziri Nape amesema, idadi ya watoa huduma wa miundombinu ya mawasiliano imefikia 25 ikilinganishwa na watoa huduma 23 waliokuwepo hadi Mwezi Aprili 2023, sawa na ongezeko la asilimia 8.7.

Maendeleo haya yanaonesha

**... leo mjadala utakamilika na hivyo wabunge wanatarajia kupiga kura kuikubali au kukataa Bajeti hiyo ya serikali. Lakini kumbuka kama wabunge wataipigia kura ya 'hapana' kwa asilimia kubwa, jambo ambalo halitegemewi kutokea, Rais Samia Suluhu Hassan atalazimika kulivunja Bunge.**

kwamba suala la malipo yasiyotumia pesa taslimu yanawezekana kwa zaidi ya nusu ya Watanzania na hadi kufikia mwaka kesho kutakuwa na ongezeko kubwa zaidi.

**MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI**

Moja ya eneo ambalo wabunge wamelizungumzia sana ni la matumizi mabaya ya pesa za serikali na wapigaji wa 'madili' huku mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby akisema kuwa wapigaji wa fedha za umma wamekuwa wengi, na wamejikita kwenye kusifia kuwa 'Mama Anaupiga Mwingi,' lakini kiuhalisia wao ndio wanaoupiga mwingi kwa kuiba fedha za umma!

"Nchi imefikia wakati sasa hivi, lazima tuseme ukweli, wapigaji wamekuwa wengi. Wengine utasikia tu, 'Mama Anaupiga Mwingi,' sio kwamba anaupiga mwingi anamsifia kwenye moyo, anaupiga mwingi yeye anaiba hela," ameeleza.

Mbunge huyo amehoji Serikali kushindwa kutekeleza ahadi yake ya kukopesha magari kwa watumishi wa umma wanaostahili kupewa magari, badala ya Serikali kubeba mzigo wa kuwanunulia ni kugharamia magari kama njia ya kupunguza matumizi ya Serikali.

Wabunge pia wamehoji ununuzi wa mashangingi, hususani kwenye halmashauri huku nyingi bado zikitegemea ruzuku kutoka serikali kuu kujiendesha.

Mbunge wa Viti Maalumu, Anatropia Theonest ameonesha kwamba baadhi ya magari yanayonunuliwa hadi shilingi milioni 300, yakifanya kazi kidogo, tuseme miaka miwili kisha yakiharibika kidogo yanatelekezwa na yanapouzwa kwenye minada yanauzwa bei ya kutupwa.

Mbunge huyo anasema ili serikali ifanikiwe katika mipango yake ni lazima sehemu kubwa ya mapato yake iende kwenye matumizi ya maendeleo, na kiasi kidogo kwenye matumizi ya kawaida, na si kama ilivyo sasa na kuonekana kushangazwa na kiasi kikubwa kinachotumiwa na serikali kwa ajili ya kununua magari kwa ajili ya viongozi.

"Unapopeleka magari ya zaidi ya shilingi milioni 800 kwenye halmashauri moja, value for money (thamani ya pesa) tunayoipata ni kiasi gani?" Amehoji Anatropia na kuongeza, "Kwa nini viongozi watumie mashangingi?"

**SUKARI**

Kuhusu sukari, serikali inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Sukari, Namba 6 ambapo pamoja na mambo mengine inalenga kuuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua, kuratibu na kuhifadhi pengo la sukari kwenye hifadhi ya chakula ya Taifa. Lengo la hatua hiyo ni kuwezesha upatikanaji wa sukari nchini na kuondoa uhodhi kwa baadhi ya wenye viwanda bila kuathiri dhamira ya serikali ya kulinda viwanda vya ndani.

Kumekuwa na maoni mchanganyiko kutoka kwa wabunge waliochangia eneo hili lakini wengi wao wameunga mkono mpango huo ili kulinda mwananchi.

Mbunge wa Tandahimba, Katani Katani alisema; "Leo hii nitashangaa kuona mbunge ambaye atapinga kuletwa sheria hii bungeni, ili wananchi wetu waendelee kupata shida kila mwaka ya kupanda kwa bei ya sukari," huku Mbunge wa Makete, Festo Sanga akisema mabadiliko ya sheria ya sukari yatasaidia kuondoa tabia iliyojengeka kwa wale waliopewa dhamana kufanya mambo kwa maslahi yao binafsi.

**GESI**

Kuhusu tozo ya shilingi 382 kwenye kila kilo moja ya gesi inayotumika kwenye magari, wabunge wengi wamepinga pendekezo hili.

Kutokana na ongezeko hilo kilo moja ya gesi kama serikali haitaachana na hatua hii, bei itakuwa Sh 1,932 kutoka Sh 1,550 iliyokuwa inauzwa awali.

Kwa upande wake, Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma amesema ongezeko hilo litakwamisha lengo la kutaka kuwe na matumizi makubwa ya nishati salama ya gesi ambayo ni kipaumbele cha Rais Samia Suluhu.

Kwa upande wake Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage alisema, "Tumekosea, na Mheshimiwa Waziri Mwigulu unisikilize, kwa nini unaweka ongezeko la pesa kwenye gesi, kwa nini gesi na watu wengi hawataki kuzungumza. Sisi gesi kwetu ni kinga, ni usalama kwamba endapo kuna tatizo kwenye ugavi sisi nchi tutabaki salama."

Akaendelea: "Dawa ni kuwahimiza Watanzania watumie gesi nyingi tuwape kichocheo kusudi, moja tuwe salama kwa vyombo vya usafiri, pili itakapotokea tatizo tutakuwa hatuna tatizo lakini mnatafuta pesa mbona mnaziacha zinapita."

Wabunge wameona pia kuweka kodi kutapunguza hamasa ya wenye magari kuhamia kwenye nishati hiyo ambayo pia ni rafiki wa mazingira.


Mbunge wa Viti Maalumu, Esther Matiko ameshauri kuharakisha kuwezesha magari ya dizeli nayo yawekewe mfumo wa kutumia gesi kwani sasa magari yanayowekewa mfumo wa gesi ni ya dizeli pekee.

Mbunge huyo pia ameshauri vifaa vinavyotumika kubadilisha mifumo ya mafuta kwenda kwenye gesi pia ipunguziwe kodi au kuondolewa kabisa ili kufanya urahisishaji wa gharama za kubadilisha mifumo na hivyo Watanzania wengi kuweza kwenda kwenye gesi.

Halikadhalika ameshauri kuongeza idadi ya vituo vya kuuza gesi asilia kwa ajili ya magari na pia kuongeza maeneo yanayowezesha kubadilisha mfumo wa mafuta kwenda kwenye gesi.

**KIKOKOTOO**

Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), limepongeza serikali kwa kuongoza malipo ya mkupuo ya pensheni kutoka asilimia 33 ya sasa hadi 40 kwa wafanyakazi waliokuwa wakilipwa asilimia 50 (PSSSF) kabla ya mifuko kuunganishwa. Aidha, mapendekezo hayo yanasema asilimia 35 iwe kwa watumishi ambao walikuwa wakipokea asilimia 25 (NSSF) kabla ya mifuko kuunganishwa.



Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba.

Lakini Tucta imeishauri serikali kuangalia upya na kuweka usawa katika nyongeza ya mkupuo ya kikokotoo kwa watumishi walioguswa na mabadiliko ya Sheria ya Utumishi wa Umma, ili kuwe na usawa wa asilimia 40 na kuondoa tofauti iliyopo.

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, anasema watumishi wote ni kundi moja la wafanyakazi wanaotoka kwenye utumishi wa umma kupitia mfuko wa PPF ambao uliunda mfuko wa PSSSF.

Nyamhokya anasema Tucta inaishauri serikali kufanya mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Sekta Binafsi, kutokana na mabadiliko yaliyopendekezwa kutonufaisha wote na kuigusa PSSSF pekee inayopata asilimia 40 huku NSSF ikiwa imepata asilimia 35.

Kwa upande wao, wabunge wa viti maalum, Halima Mdee na Esther Bulaya wamesema kuwa suala la serikali kuongeza malipo ya mkupuo ya pensheni hadi asilimia 40 bado hayatoshi, badala yake wameitaka serikali kama kweli ina dhamira ya kuboresha maslahi ya watumishi warejeshe bungeni sheria hiyo ifanyiwe maboresho, pamoja na kanuni zake ili kuwanufaisha watumishi.

"Sote tunajua kikokotoo bado ni janga na hii haijaisha mpaka iishe. Hitaji lao lilikuwa asilimia 50 wachukue mafao kwa mkupuo," amesema Bulaya.

**SHERIA YA KODI**

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba amepinga mpango wa serikali wa kurekebisha Kifungu cha 86(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kwa kuweka ukomo wa faini ya juu ya kosa la kutokutoa risiti wa kiasi cha shilingi 15,000,000. Amesema anayeuza bidhaa sio tajiri bali ni mfanyakazi, hivyo amehoji kwa nini mfanyakazi afanye kosa halafu adhabu apewe tajiri ambaye hafahamu kilichotokea. Pia, amependekeza mtu ambaye atanunua bidhaa au kulipia huduma na asipodai risiti naye apewe adhabu.


Sukari.


Mashangingi

# Msoga Half Marathon, jambo jema la kuigwa




**Lengo ni kuchangisha fedha kiasi cha shilingi milioni 700 ili kuboresha huduma ya mama na mtoto kwenye Hospitali ya Wilaya ya Msoga kwa kununua vifaa tiba vitakavyotumika kwenye wodi ya wazazi na mtoto njiti.**

**Na Dk. Reubeni Lumbagala**

Nayakumbuka vyema maneno ya mwalimu wangu wa Somo la Uraia takribani miaka 20 iliyopita nilipokuwa kidato cha kwanza.

Mwalimu huyo wakati akitufundisha mada ya Haki za Binadamu alitutolea mifano ya haki mbalimbali kuhusu haki hizo kama vile haki ya kusikilizwa, haki ya kuchagua na kuchaguliwa, haki ya kujiunga na taasisi uitakayo, haki ya kujieleza, haki ya kupata elimu, haki ya kucheza, haki ya kuishi na haki ya kulindwa, kutaja kwa uchache.

Lakini katika mkazo wake, mwalimu alituambia pamoja na kwamba haki zote za binadamu ni muhimu sana lakini haki ya kuishi (Right to life) imebeba haki nyingine zote.

Kivipi? Kimsingi, binadamu anapokuwa hai anakuwa na nguvu ya kudai haki zake nyingine zote ili aweze kuzipata na kuzifurahia. Akatusisitiza kuwa kama ni suala la kuzipanga haki za binadamu kimtiririko kutokana na uzito wake, basi haki ya kuishi ni namba moja, nyingine zinafuata. Ndiyo maana hata wanaopinga adhabu ya kifo, wanazo sababu nyingi lakini pamoja na kusema kwamba wapelelezi, waendesha mashtaka hadi hakimu anaweza kukosa na hivyo mkanyonga mtu asiye na kosa na kumnyofoa haki namba moja ambayo hamwezi kumrejeshea tena uhai hata mkigundua makosa baadaye.

Kwamba mtu hata afanye kosa lipi ikiwemo kuua, ukishamnyonga, anakosa nafasi ya kujutia makosa yake au kutumikia adhabu nyingine mbadala itakayomfanya ajutie kosa lake. Makala hii hailengi kuzungumzia haki za binadamu kwa kina bali nimeyakumbuka maneno haya ya mwalimu wangu kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa sekta ya afya kwani sekta ya afya ni miongoni mwa sekta ambazo zina uhusiano wa moja kwa moja katika kuhakikisha binadamu anapata haki ya kuishi kupitia huduma bora za afya zinazoweza kuokoa maisha yake pale anapoumwa.

Ndiyo maana unaweza kumsikia Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel, akijibu swali bungeni kama ilivyotokea juzi kwamba Tanzania imefanikiwa kupunguza vifo vya mama na mtoto kabla ya muda uliotegemewa na kuvunja rekodi ya kufikia 104 badala ya 225 iliyotegemewa mwaka 2025.

Kwamba kitaifa vifo vimepungua kutoka 556 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2023 ambapo kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ilitegemewa vifo vipungue hadi kufikia 225 ifikapo mwaka 2025.

Nini kinapunguza vifo hapo? Jibu bila shaka ni kuboresha huduma bora za afya na kuchangia binadamu kupata haki ya kuishi na kufurahia maisha yake kwa kupata tiba na matibabu bora.

Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitaja maadui watatu wa maendeleo akisema ni ujinga, umaskini na maradhi na akaweka mkazo mkubwa kwa Watanzania kupambana kutokomeza maadui hawa kwani bila kufanya hivyo, itakuwa ngumu kufikia maendeleo endelevu. Adui maradhi atatokomezwa kupitia elimu na huduma bora za afya kwa wananchi.

Maradhi, hata kama hayapotezi haki ya mgonjwa kuishi lakini yanasababisha watu kushindwa kuzalisha mali ipasavyo, na si kwa mgonjwa pekee bali hata wanaomuuguza.

Kutokana na umuhimu wa kuwa na afya bora, serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kama wale wa kusaidia maendele (development partners), taasisi za dini, sekta binafsi na wengineo katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya katika ngazi zote kuanzia kwenye zahanati, vituo cha afya, hospitali za wilaya, mkoa, rufaa hadi taifa.

Huduma ya mama na mtoto kama aliyoigusia Naibu Waziri Molle juzi bungeni, ni muhimu sana kwani bila kuweka mazingira bora ya afya, kundi hili litakosa kufurahia haki ya kuishi kwani ukosefu wa huduma au huduma mbovu dhidi yao husababisha vifo vyao, jambo ambalo serikali au mtu yeyote makini hawezi kuwa tayari kuliona likitokea na ndiyo maana serikali inapambana asubuhi, mchana, jioni na usiku kutokomeza vifo vya mama na mtoto.

Ikumbukwe kwamba kiwango cha vifo vya watoto wachanga pekee kinachukuliwa kuwa kipimo nyeti sana cha afya ya idadi ya watu kwa sababu kuna uhusiano kati ya sababu za vifo vya watoto wachanga na mambo mengine ambayo huathiri hali ya watu wote kama vile maendeleo ya kiuchumi, hali ya jumla ya maisha, ustawi wa kijamii, viwango vya magonjwa na kadhalika.

Serikali inapambana kuitokomeza hivi hivi kwa kuwekeza fedha nyingi ili kuhakikisha mama na mtoto wanapata huduma bora za afya.

Juhudi za kuboresha huduma ya mama na mtoto zinafanyika nchi nzima ili kuhakikisha mama na mtoto wanakuwa salama kwa kupata huduma bora za afya.

Kwa upande wake, Mbunge wa Chalinze (CCM) ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, ameipa kipaumbele sekta ya afya. Hii ni kwa sababu pamoja na mambo mengine, anafanya jitihada kubwa kuhakikisha ubora wa huduma ya mama na mtoto jimboni kwake inakuwepo kwa ubora na viwango vya juu.

Kutokana na umuhimu wa raslimali fedha katika uboreshaji wa huduma hiyo, Ridhiwani kwa kushirikiana na viongozi na wadau wa maendeleo wameandaa mbio za hisani zilizopewa jina la "Msoga Half Marathon 2024" zitakazofanyika Jumamosi Juni 29, 2024, kuanzia saa 12 asubuhi katika viwanja vya Msoga, Chalinze.

Lengo ni kuchangisha fedha kiasi cha shilingi milioni 700 ili kuboresha huduma ya mama na mtoto kwenye Hospitali ya Wilaya ya Msoga kwa kununua vifaa tiba vitakavyotumika kwenye wodi ya wazazi na mtoto njiti (watoto wanaozaliwa kabla ya wakati).

Hebu fikiria, ingawa kama nchi tumepunguza sana vifo vya mama na mtoto (rejea jibu la Naibu Waziri wa Afya bungeni) lakini hatua hii ya Ridhiwani inaenda kuokoa vifo vingapi? Mbio hizo zitahusisha watu kukimbia umbali wa kilometa 5, 10 na 21. Kwa yeyote aliye tayari kushiriki mbio hizo anaweza kujisajili kwa kulipia gharama za usajili kiasi cha shilingi 35,000.

Lakini kwa ambaye hataweza kushiriki katika mbio hizo, yuko huru kuchangia kiasi chochote kadri alivyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Kama ambavyo nimeshagusia awali, upatikanaji wa fedha hizo utasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya mama na mtoto na hatimaye kuwahakikisha usalama na haki yao ya kuishi kupitia huduma bora za afya.

Wakati nikihimiza watu wengi kujitokeza kuchangia mbio hizo kutokana na faida itakayopatikana na hata wahusika kupata thawabu kutoka kwa Mungu Mwenyezi kwa kufanya jambo la kuokoa maisha ya viumbe wake, kwa mtazamo wangu, haya ndio mambo mazuri ya wengine kuiga.

Nasikia mwisho wa wiki pale Morogoro, ile mechi ya Timu Kibwana na Timu Job ililenga pia kuchangia huduma za kitiba za mama na mtoto. Ni ubunifu mzuri na hivyo kinachotakiwani ni watu, kila sehemu kuendelea kuwa wabunifu kupata fedha za kuokoa mama na mtoto huku sisi wengine tukiunga mkono kwa dhati juhudi kama hizi kwa kuchangia na sisi waandishi wa habari na makala kuendelea kuhamishia jamii kuunga mkono juhudi hizi.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti, ama kama wabunge wanavyopenda kusema kwamba 'kasungura kadogo' serikali haiwezi kuboresha huduma za mama na mtoto kwa asilimia 100 nchi nzima. Afua kama hizi ni muhimu.

Ndio maana nahimiza viongozi wengine katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kuja na mipango inayoshirikisha wadau mbalimbali katika kuboresha huduma za afya.

Nimalizie kwa kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameanzisha utaratibu wa madaktari bingwa kutembelea mikoa mbalimbali kutibu wananchi (Maarufu Madaktari wa Samia) kwa kushirikiana na madaktari wa eneo husika na juzi wameanza kazi mkoani Mara. Na Moja ya eneo watakaloliangalia kwa umakini ni hili la afya ya mama na mtoto.

Halikadhalika ninampongeza Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ambaye amefanikiwa kukusanya madaktari lukuki na vifaa tiba na kuweka kambi ya kutoa huduma za afya kwa wana-Arusha huku vipimo na ushauri vikitolewa bure kabisa.

***Dk. Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0620 800 462***

# Heshima kubwa wafuga nyuki duniani kote kukusanyika Tanzania 2027



**Na Thomas Chale**

Bila shaka ulishawahi kusikia neno Apimondia, siyo? Kama hujawahi basi usipate taabu. Nitakufafanulia. Hili ni shirika la kimataifa lisilo la kiserikali linalowaleta pamoja wafugaji nyuki, watengenezaji wa vifaa vya ufugaji nyuki na wanasayansi mbalimbali wanaojihusisha ufugaji nyuki (apiculture), tiba zitokanazo na asali (apitherapy), uchavushaji, maendeleo ya biashara zinazohusisha nyuki na uchumi utokanao na nyuki kwa ujumla.

Lengo la shirika hili ni kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa na mijadala ambapo wafugaji nyuki, wanasayansi, wafanyabiashara wa asali, mawakala wa maendeleo ya shughuli za nyuki, mafundi na wabunge hukutana kusikiliza, kujadiliana na kujifunza kutoka kwa kila mmoja wao.

Kwa hiyo, mbali na maana hiyo kwamba ni shirika, lakini Apimondia huchuliwa zaidi kama kusanyiko muhimu sana la kimataifa ambapo wafugaji nyuki na wadau wengine wa nyuki duniani hukutana pamoja.

Kama nilivyokwishadokeza lengo la kujadili ni kufanya biashara ya mazao ya nyuki na teknolojia zake. Pia kupata taarifa za kisayansi za tafiti mbalimbali zihusuzo nyuki.

Mkutano wa kwanza ulifanyika mwaka 1897 katika mji wa Antwerp, Ubelgiji, kisha ukawa unazunguka kila baada ya miaka miwili kwenye nchi nyingine na ifikapo 2027 utafanyika Arusha Tanzania.

Tanzania iko tayari kuwa mwenyeji wa Apimondia 2027, itakayofanyika Katika kituo cha Mikutano ya Kimataifa AICC Arusha Tanzania, ambapo zaidi ya wageni 6,000 wanatarajia kuhudhuria.

Hayo yalithibitishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kariuki alipokuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonesho ya kwanza ya asali Tanzania (Honey Show), yaliyofanyika Juni 19-21, 2024 katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Katika hafla hiyo, Waziri Angela Kiriuki, aliambatana na Rais wa Apimondia Duniani, Dk. Jef Pettifs, Rais wa Apimondia Kamesheni ya Afrika Bw. David Mkomana na Waziri Mkuu Mstaafu, mtoto wa Mkulima Mizengo Kayanza Pinda. Waziri Mkuu Mstaafu, Pinda ni mmoja wa wafugaji wakubwa wa nyuki nchini Tanzania

Waziri Kariuki alieleza lengo la maonesho hayo kuwa ni kutoa elimu ya umuhimu wa sekta ya nyuki, uongezaji thamani mazao ya nyuki, nafasi yake katika utunzaji mazingira, ukuzaji uchumi, uongezaji ajira, tiba na lishe.

Waziri Kariuki, aliwapongeza sana waandaaji wa maonesho hayo ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ikiongozwa na Kamishina wake Prof. Dosantos Silayo kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi ikiwemo TanziFarm iliyowakilishwa na Mhandisi Kaizirege Kamara.

Wadau wengine walioshiriki na kuwezesha na kufanikidha maonesho hayo ni Benki ya CRDB, NMB na shirika la mikopo ya karadha la PASS, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau wengine kadha wa kadha.

Waziri Kariuki alihamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kuchangamkia fursa za ufugaji nyuki na uzalishaji wa asali ili kukuza vipato vyao.

Waziri Mkuu mstaafu, Pinda, ambaye pia ni mlezi wa shughuli za ufugaji nyuki, alipongeza sana sekta binafsi, ampapo vijana wengi walionesha mfano wa kuigwa katika sekta na taasisi zisizo za kiserikali kwa pamoja katika utayari wa kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya nyuki.

Waziri Kariuki alimhakikishia Rais wa Apimondia na wadau wengine kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Hassan Suluhu ameridhia mkutano wa Apimondia 2027 kufanyika Tanzania na kwenye ukumbi wa AICC ulioko katika Mji wa kitalii wa Arusha.

Tanzania ambayo kwa sasa inazalisha tani 35,000 za asali kwa mwaka, inalenga kuongeza uzalishaji hadi kufikia hadi tani 100,000 kwa mwaka.

Maonesho hayo yaliyomalizika Ijumaa ya wiki iliyopita yakiwa na kaulimbiu "Beyond Hives, Beyond Borders" yalishrikisha wadau kutoka, Uingereza, Hispani, Misri, Zimbabwe, Lesotho, visiwa vya Ushellishelli na Kenya.

Akitoa shukrani zake kwa dhati, Dk. Jeff, Rais wa Apimondia alisema, haikuwa rahisi kwa Tanzania kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo mkubwa duniani, ambapo nchi saba ziliwania kupata wasaa huo na zilishindana na mwisho ikabaki Tanzania na Umoja wa falme za Kiarabu (UAE).

Hii ilikuwa Septemba 2023 mjini Santiago Chile, kura zilipigwa na Tanzania ikachaguliwa, pongezi kwa viongozi wa Wizara na bosi wa TSF, Prof. Silayo na timu yake iliyowakilisha Tanzania vizuri katika mkutano ule wa Santiago, Chile.

Hivyo Tanzanzia itakuwa mwenyeji wa mkutano wa 50 wa Apimondia baada ya mkutano wa 49, utaofanyika Copenhagen, Denmark, mwaka 2025.

Ugeni wa watu takribani 6,000 si haba kwani ujio wao utawanufaisha Watanzania wengi wakiwemo wafanyabiashara mbalimbali na wenye mahoteli. Bila shaka wageni hawa watapata pia fursa ya kutembelea vivutio vyetu vya utalii na hivyo kwenda kuwa wapiga debe wetu wazuri wa vivutio vya Tanzania.

Shime wakazi wa Arusha, 2027 unaweza kudhani ni mbali lakini ni keshokutwa tu. Ninaamini mtaendeleza ukarimu wetu kama Watanzania kwa wageni wetu hawa.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Ujumbe maridhawa kwa wanachama wa CCM




Lengo la chama chochote cha siasa ni kushika dola kwa maana ya kushinda uchaguzi mkuu na hatimaye kuunda serikali. Hata hivyo, ili chama cha siasa kiweze kushinda uchaguzi mkuu ni lazima kijipange ipasavyo kwa kuongeza idadi ya wanachama, kufanya mikutano ya hadhara kwa kunadi sera zake ili kujiimarisha zaidi na mwishoe wananchi wakichagüe kupitia sanduku la kura siku ya uchaguzi.

Ushindi wa chama chochote cha siasa hauji kwa miujiza bali ni matokeo ya kujipanga na kujiimarisha kisiasa na kuwa na sera nzuri zinazotekelezeka na zinazogusa maisha ya wananchi. Kwa hiyo, vyama hivi vya siasa, iwe ni chama tawala au vyama vya upinzani, vina kazi kubwa ya kufanya ili kuweza kushinda uchaguzi.

Wajibu wa kuhakikisha chama kinashinda uchaguzi ni jukumu la viongozi pamoja na wanachama, wafuasi, wakereketwa, mashabiki wa chama husika. Chama kinapofanikiwa kushinda katika uchaguzi, ushindi huo ni fahari na heshima kwa viongozi na wanachama.

Kwa mantiki hii, ni lazima viongozi wawe bega kwa bega na wanachama wao na kushawishi wanachama wapya katika kutafuta na kufanikisha ushindi. Hakuna ushindi unaoweza kupatikana kwa juhudi za viongozi pekee au wanachama pekee, ni lazima viongozi na wanachama waunganishe nguvu ya pamoja kuusaka ushindi na ndiyo maana wahenga walisema umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

Ni bahati mbaya wakati mwingine, baadhi ya wanachama wanadhani vyama vyao vinaweza kushinda kwa juhudi za viongozi pekee. Hapana. Mwanachama wa chama chochote cha siasa anao wajibu wa kujitoa ipasavyo ili kuchangia ushindi wa chama chake katika uchaguzi. Kujitoa na kupigania chama ndiyo chachu ya uimara na ushindi katika uchaguzi.

Kimsingi, mwanachama anapaswa kujitoa kikamilifu kwa chama chake, mathalani, kuhudhuria vikao, mikutano, kutoa mchango wa mawazo, mapendekezo, fedha na hata kuuza sera za chama chake kwa wananchi ili kuongeza idadi ya kura na hatimaye chama chake kiweze kupata ushindi wa kishindo.

Hivi karibuni, Mbunge wa Jimbo la Chalinze kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete alikuwa mgeni rami kwenye Mkutano wa Kuwaaga Wanachama wa CCM, Seneti ya Vyuo na Vyuo Vikuu. Mkutano huu ulifanyika katika Chuo cha Mtakatifu Jordan mkoani Morogoro.

Katika hotuba yake aliyoitoa, pamoja na mambo mengine, aliwaasa vijana wa CCM kukipigania chama chao kwa wivu mkubwa ili kulinda na kutekeleza malengo na kuleta maendeleo kwa wananchi bila ubaguzi.

"Piganieni chama chenu, msisubiri kukumbushwa jukumu hilo," alisema Ridhiwani. Huu ni ujumbe mfupi na ambao unaweza kuonekana wa kawaida lakini ukiuchambua unaweza kujaza madafatari kadhaa ya kurasa 48! Ujumbe huu unaweza kufanyiwa kazi si WanaCCM pekee waliohudhuria hafla hiyo lakini pia kwa wanachama wengine nchi nzima.

Kimsingi, Ridhiwani Kikwete anaelewa nguvu ya wananchama katika kufanikisha ushindi. Pamoja na kwamba alikuwa anaongea na vijana lakini ushindi wa CCM unategemea pia mchango wa jumuiya ya wanawake, wazazi, wakereketwa, mashabiki, wafuasi wa CCM na wananchi kwa ujumla.

Kutokana na umuhimu wa wanachama kupigania chama chao, ni kweli kabisa hakuna sababu ya wanachama kusubiri kuambiwa na viongozi wao wajibu huu wa msingi bali wao wenyewe wanatakiwa waanze mchakato huo kwa kutambua kuwa bila juhudi zao hakuna ushindi.

Vijana ni nguvu kazi ya Taifa. Kwa hiyo, hata katika harakati za kupigania chama, vijana wanayo nafasi kubwa ya kutoa mchango wao na hatimaye kufanikisha ushindi wa kushindo bila kusahau kushirikiana na wengine. Wito uliotolewa na Ridhiwani Kikwete juu ya wanachama wa CCM kupigania chama chao umekuja wakati mwafaka ikizingatiwa kuwa mwaka huu kuna uchaguzi wa serikali za mitaa na mwakani uchaguzi mkuu.

Katika chaguzi hizi, CCM kinakwenda kueleza yale waliyoyaahidi kipindi cha uchaguzi na yapi wameyatekeleza. Aidha, CCM kinakwenda kuomba ridhaa kwa mara nyingine kuendelea kuwatumikia wananchi.

Ni wajibu sasa wa kila mwanachama wa CCM kuangalia namna ambavyo ataweza kusaidia ushindi wa chama chake badala ya kukaa sebuleni na kuimba "Iyena iyena, shangilia ushindi unakuja" bila yeye kuwajibika kujitoa kwa hali na mali kutafuta ushindi wa chama chake. Mwanachama anaweza kutoa msaada wa kimawazo (moral supports) au msaada wa vitu (material supports) ili mradi kufanikisha ushindi wa chama.

Yapo mengi ambayo yamefanywa na serikali ambayo yanapaswa kusemwa kwa wananchi ili kuondoa upotoshaji uliopo wa baadhi ya watu wanaodai serikali haijafanya chochote. Ni muhimu wananchi wapewe taarifa sahihi kuhusiana na kazi nzuri ziliyofanywa na serikali katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Ikumbukwe kuwa uongo ukisemwa bila kukanushwa, uongo huo hugeuka kuwa kweli. Wanachama wa CCM wanalo jukumu la kutoa maelezo na ufafanuzi wa kina ili kuondoa upotoshaji uliopo kuhusiana na kazi nzuri zilizofanywa na serikali.

Kuna mitandao ya kijamii kama Facebook, Whatsapp na Instagram ambapo wanachama wa CCM wanaweza kuitumia kueleza na kufafanua kazi nzuri zilizofanywa na serikali zinazogusa maisha ya watu kwenye sekta za afya, elimu, maji, umeme, miundombinu, kilimo, biashara, masoko, viwanda, uvuvi, na mifugo.

Aidha, kwa wale wenye uwezo wa kuandika makala na uchambuzi wa kina wa miradi mbalimbali ya maendeleo na ile ya kimkakati iliyotekelezwa na serikali wanaweza kuandaa makala hizo ili ziweze kusomwa na wananchi mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii, magazetini na kwenye majarida ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusiana na kazi nzuri zilizofanywa na serikali yao sikivu.

Hii yote ni namna ambayo wanachama wanaweza kupigania chama chao ili kiendelee kupata ridhaa ya wananchi ya kuwaongoza katika kipindi kingine cha miaka mitano ijayo.

Viongozi wa chama wanao wajibu wa kuwapa wanachama wao taarifa sahihi za miradi mbalimbali ya maendeleo na ya kimkakati pamoja na thamani ya fedha za miradi hiyo iliyotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ili wanachama wawe na ujasiri wa kueleza na kukipigania chama chao mbele ya wananchi. Aidha, kuna umuhimu wa wanachama kuelewa namna miradi hiyo ya maendeleo ilivyosaidia kuboresha maisha ya wananchi, hii itasaidia kujenga na kuendeleza imani ya wananchi kwa chama.

Naamini ujumbe mzuri uliotolewa na Ridhiwani Kikwete utafanyiwa kazi na wanachama na viongozi wote wa CCM. Mapenzi ya wanachama na viongozi kwa chama chao ni pamoja na kukipigania kwa hali na mali, iwe jua iwe mvua, kwa jasho na damu ili kiendelee kupata ridhaa ya kuongoza. Wito mzuri umetolewa, kifuatacho ni kuingia kwenye utekelezaji mara moja yaani chap kwa haraka..

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

# Dondoo za matumizi sahihi ya muda



Matumizi sahihi ya muda (time management) ni moja ya mambo muhimu kuyazingatia ili kufikia hatma unayoikusudia. Watu wengi wamekuwa wakiimba dhana hii bila mafanikio na kujikuta wakipoteza muda mwingi kwa vitu visivyo na maana.

Tunapoongelea matumizi sahihi ya muda ni kuhakikisha muda wako unatumika kwenye vitu ulivyopanga na vinavyokuletea matokeo. Leo Kliniki ya Fikra inaangazia dondoo muhimu zitakazokusaidia kutumia muda wako vizuri. Tafadhali Fuatana nami: -

## KUWA NA MPANGO WA MAMBO YAKO (PLAN)

Watu wengi wanaishi na kufanya mambo yanayokuja tu. Ni muhimu kupanga siku zako na kuhakikisha kila muda upo kwenye mpangilio. Ukiweza kupanga ni hatua kubwa kukufanya utumie muda wako vizuri.

Andaa ratiba yako ya siku, wiki au mwezi na hata mwaka ukionesha mambo muhimu kwa wakati husika, utayafanya lini na kwa rasilimali zipi? Hakikisha una orodha ya mambo yako ya kufanya kila siku (To do List). Tumia kalenda mtandao (Kama vile google calendar), weka vitu vya kukukumbusha kama (reminders, alarm, nk.) Dalili ya mtu kufanikiwa ni pamoja na kuwa na mpango mzuri wa mambo yake.

## KUWA NA VIPAUMBELE

Baada ya kuwa na orodha ya mambo ya kufanya, ni muhimu kuweka vipaumbele ili kujua nini kinaanza na kipi kinafuata. Ni muhimu ukiamka tu, uwe unajua ninaanza na nini na kinachofuatia ni nini?

## ANZA MAPEMA

Hii ni siri itakayokupa hamasa ya kutumia muda wako vizuri. Ili kufanikisha hili: lala mapema, lala saa za kutosha zinazoshauriwa kitaalamu, na ndipo utafanikiwa kuamka mapema na kuanza ratiba zako mapema. Pia ili ufanikiwe vizuri kwenye majukumu yako, anza kwa sala (maombi), anza na mazoezi mepesi kisha anza na mambo rahisi ili kukupa hamasa.

## CHANGANUA KILA JUKUMU LAKO

Ukipata jukumu la kufanya, lichanganue vizuri. Mfano ukiweka lengo la mwaka ni kujenga nyumba, basi anza kuchanganua lengo hilo kwenye "tasks" ndogondogo kama vile, lini unatakiwa kununua kiwanja, mpaka lini utanunua matofali, unahitaji simenti mifuko mingapi, nondo ngapi, mbao kiasi gani, gharama ya ufundi ipoje, bati, milango, madirisha, umeme, bomba, nk.

Hapa utakuta ndani ya lengo moja kubwa, kuna kazi au malengo madogo mengi. Haya yatakupa kujua sasa uhalisia wa ugumu au wepesi wa jukumu lako.

## GAWA MAJUKUMU (DELEGATE TASKS)

Kama upo na watu, ni vizuri sana ukigawa majukumu. Usilazimishe kufanya kila kitu mwenyewe. Hii itakupa faida nyingi kama kukamilisha mambo kwa haraka, kurithisha uwezo, kuwapa nafasi wengine kukua, itakuongezea uzoefu wa usimamizi, nk.

## WEKA MALENGO JANJA (SMART GOALS)

Malengo yako ili yatimie hakikisha ni malengo mahsusi (specific), yanayopimika (measurable), yanatekelezeka (achievable), ni malengo halisia (realistic) na pia yawe na muda maalumu na ukomo (time bound). Malengo yenye sifa hizi, hayatakupotezea muda kwenye kuyasimamia kutimia.

## USITOKE NJE YA MALENGO (AVOID DESTRUCTION)

Ukishaweka malengo ni muhimu sana kuwa makini na mwangalifu ili usitoke nje ya malengo. (Hii inaitwa "Focus" Usianze kuvutiwa au kutamani malengo ya watu. Mfano mfano kwenye mitandao ya kijamii, maongezi, wageni wengi na marafiki, kupokea majukumu ya kusaidia na kutamani njia za watu

## SEMA HAPANA KWENYE BAADHI YA MAMBO

Ili ufanikiwe kutumia muda wako sawasawa lazima uwe na uwezo wa kusema hapana kwenye mambo ambayo hayapo kwenye ratiba zako na hususan yale ambayo hayana mchango chanya kwenye malengo yako.

## SHUGHULIKIA MSONGO WA MAWAZO (AVOID STRESS)

Ili kutumia muda wako vizuri shughulikia mambo yanayoweza kukutia kwenye msongo wa mawazo au kama tayari upo kwenye hilo tatizo basi shughulikia kwa hekima. Msongo wa mawazo una tabia ya kumpotezea muda sana mhusika na kumwacha kwenye njiapanda kwa muda mrefu.

## USIFANYE MENGI KWA WAKATI MMOJA (MULT-TUSKING)

Pamoja na kuwa utafiti unaonesha kuwa wanawake wanaweza kufanya mambo kadhaa kwa wakati mmoja, lakini ni vizuri sana ukafanya jambo moja kwa wakati mmoja. Hii itakujenga zaidi kuliko kuwa na mambo mengi kwa wakati mmoja.

## PUMZIKA

Ukitaka kuwa na matumizi mazuri ya muda, pumzika. Pumzika katikati ya kazi ili kurudisha umakini (Time off – 5 minutes room), fanya mapumziko ya mwili na jiburudishe (refreshments).

## FUATILIA UTIMIZAJI WA MALENGO

Hii itakufanya usisubiri hadi mwisho wa kazi kugundua kuwa kazi zote zimeharibika uanze upya. Fuatilia kwa nyuma kuhakikisha kila kitu kinaenda vyema na mambo ya kurekebisha, fanya mapema.

## JITATHMINI (EVALUATION)

Hili ni jambo muhimu sana kwenye kutunza muda wako sababu bila kujifanyia tathmini za mara kwa mara, utajikuta unarudia makosa yaleyale mara kwa mara jambo ambalo ni upotevu mkubwa wa muda.

Wework Consult - Your Partner in Growth

# Ziara Chadema zinavyompaisha Samia

*Inatoka uk. 11*

Tunataka kusikia wao wataboresha vipi eneo hilo. Je, sasa watakuja na elimu bure mpaka chuo Kikuu? Kwenye afya vipi? Madini, kilimo, ufagaji, uvuvi, utunzaji wa mazingira na mengine lukuki wao wamejipangaje?

Hizi siasa za kupakana matope kama njia ya kuamini zitakupa wachama wengi mimi naamini ni kujichora tu.

### KUPOTEZA MUDA

Utatumia maneno yapi mapya ya kumpaka matope Dk. Samia mbele ya Watanzania hivi sasa? Bila shaka ni kupoteza muda. Kazi za Mama huyu wa Taifa zinaonekana na kila raia wa taifa hili wakiwemo wale wavaa miwani ya mbao kama baadhi ya viongozi wa Chadema.

### UKABILA

Katika ziara yao hiyo ya mikoa ya Kaskazini, pia Chadema wanaendelea kujadili Uzanzibari wa Rais Dk. Samia na kueneza uongo kwamba kutokana na kutoka huko upande wa pili wa Muungano wa taifa hili ndiyo maana hana uchungu na mikoa hiyo kiasi cha kuamua kuuza ardhi yao kwa Waarabu wa Omani!

Wanaoeneza hii sumu ya ubaguzi si wengine ni bali wale wale viongozi wakuu wa chama hicho, Mbowe na Makamu wake Lissu ambao sasa suala la Rais Dk. Samia na Uzanzibari wake imekuwa ajenda yao kuu kwenye kila mkutano wao!

Hili suala la Chadema kutoukubali hata kidogo Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, halikuanza awamu hii, bali ni muda mrefu tangu wakati wa awamu za tatu na nne, lakini Rais Dk. Samia katika hotuba yake ya kwanza kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano mwaka 2021 alisema kuwa, ataupigania kwa nguvu zake zote.

Kiongozi kinara wa chama hicho anayeongoza kuhoji masuala ya Zanzibar katika Muungano wetu ni huyu Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu.

Baada ya kuipinga kwa muda mrefu Zanzibar, sasa Mwenyezi Mungu amempiga bakora ya kiutu uzima kwa kumleta Mzanzibari Dk. Samia kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

Hebu fikiri Lissu anajisikiaje kuongozwa na Mzanzibari ambako tangu awe mwanasiasa hajawahi kuukubali upande huo ingawa alikwenda kule kuomba kura zao alipogombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2020!

Lissu ni msomi aliyebobea katika masuala ya sheria na ni mmoja ya mawakili wazuri tu hapa nchini. Lakini kujitumbukiza kwake katika mambo ya kisiasa naye ameweka taaluma pembeni na kugeuka kuwa bingwa wa mazingaombwe ya kisiasa.

### HACHAFULIKI

Nimewahi kuandika kwamba, Dk. Samia hachafuliki, narudia tena kamwe Chadema hawatafanikiwa kile wanachoita kukijenga na kuimarisha chama chao kwa ngonjera za kujaribu kumpaka matope rais wetu!

Changamoto kubwa inayoikumba Chadema na vyama vingine vya upinzani ni kukosa utambulisho kwenye makundi ya kijamii na hii imetokana na sababu nyingi ikiwemo viongozi waliochoka kung'ang'ania ofisi. Vile ambavyo vimeshindwa kusimamia itikadi zao zilivyovianzisha, vivyo hivyo vyama vingi havina shabaha kwa makundi mahsusi.

Hii ndiyo imekuwa sababu ya vyama hivi kuibuka na hoja za propaganda zisizoisha, mara mafisadi papa, mara huyu si Mtanganyika; propaganda muflisi zinazowafanya wagande sehemu moja bila kupiga hatua kwenye medani za siasa hapa nchini.

Bahati mbaya kwa vyama vya upinzani nchini ni kuwa vinachuana na chama kikongwe kinachoongoza dola kwa zaidi ya miaka 63 sasa.

Utaona kuwa CCM shabaha yake ilikuwa Watanzania wanyonge, yaani wakulima na wafanyakazi. Hata hivyo, baada ya kukaa madarakani muda mrefu, kilifaidika na kikawa chama cha watu wote, yaani hadi wafanyabiashara na vigogo wenye fedha.

### CHADEMA NA UPWEKE

Ni shida kubwa kwa chama cha siasa ambacho hakijawahi kushika dola, kikiwa hakijipambanui kimaudhui kuhusu wakulima, wafugaji, wavuvi na wote wenye kuendesha maisha kupitia fursa asilia. Chama kinakuwa hakina kundi linalokishika mkono.

Vyama vya upinzani vipo vingi, lakini wamachinga, mama lishe, waendesha bodaboda, bajaji na kadhalika hawaoni chenye kutafsiri vizuri changamoto zao ili wakione cha kwao. Uchaguzi unapofika wanaangalia mvuto wa mgombea na siyo chama.

### KUPOTEZA MWELEKEO

Vita dhidi ya ufisadi ulikuwa utambulisho mkuu wa vyama vya upinzani kabla ya Uchaguzi Mkuu 2015. Utambulisho huo umeshapoteza mvuto na unaendelea kufutika kadiri Rais wa Awamu ya Sita, Dk. Samia Suluhu Hassani anavyopambana kurejesha nidhamu ya uwajibikaji na kupunguza kama si kuziba kabisa mianya ya rushwa.

Je, vyama kama Chadema havioni makundi mahsusi ya kutetea ili viungwe mkono na kupata utambulisho badala ya kuendeleza siasa za maji taka kila mwaka?

Ni hasara kubwa kwa chama cha upinzani kuifikiria dola wakati hakitafsiriki kwa unyoofu kwenye makundi ya kijamii. Matokeo yake watu wanaona vyama vipo sawa, isipokuwa vinatofautiana kuwa kingine kinatawala na vingine ni upinzani.

Chama cha upinzani kutegemea aina ya mgombea kwenye uchaguzi ili kukishinda chama tawala ni hasara kubwa. Chama kinatakiwa kiwe na mtaji mkubwa wa kuingia nao kwenye uchaguzi. Mtaji huo ni utambulisho wake kwenye jamii na namna kinavyopokelewa.

Chama hakipaswi kuingia kwenye uchaguzi na matarajio ya kamari. Kinapaswa kuwa na mtaji mzuri wa kisiasa. Na mtaji bora wenye nguvu ni utambulisho wake. Chama kikikumbatiwa na kundi kubwa au lenye mvuto na matokeo huvutia.

Kwa hiyo Chadema wajue yale wanayoyafanya hivi sasa kwenye ziara yao ya mikoa ya Kaskazini si kumbomoa Rais Dk. Samia bali ni kuzidi kumnadi yeye na chama chake CCM kuelekea uchaguzi wa mwaka huu wa Serikali za mitaa na ule Uchaguzi Mkuu wa mwakani!

***Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 au 0784 122 020.***

# Ni suala la kufa na kupona

*Inatoka uk. 10*

Tunachokishuhudia sasa ni matokeo hasi maana kwa zaidi ya miaka 60 ya uhuru; yamekuwa yakijitokeza taratibu taratibu lakini sana kimefikia kiwango hatarishi. Mvua zikinyesha mito inafurika maji haraka kiasi cha kuvuka kingo za mito na kusambaa haraka na kusababisha mafuriko yasiyotarajiwa. Vilevile, ardhi ya kufaa kilimo imekuwa ikipungua na hivyo taifa kukabiliana na athari za maeneo kadhaa kugeuka jangwa. Sasa Tanzania Bara hali ndiyo hiyo inayoyumbisha maisha yetu na vizazi vijavyo.

### TUSILEGEZE KAMBA

Nini Kifanyike? Kwanza, nashukuru kwa hatua iliyochuliwa na viongozi wa kitaifa kukemea uharibifu mkubwa wa mazingira na kuwataka Watanzania kuchukua hatua kulinda mazingira kwa kupanda miti kwa wingi pia kuitunza misitu iliyo karibu nao katika maeneo wanayoishi. Hili ni jambo jema na la kupongezwa maana ni 'Utashi mzuri Kisiasa' kama ilivyojitokeza 2014.

Tusilegeze kamba bali juhudi zipate msukumo toshelezi kiasi kwamba miti ikioteshwa inatunzwa, inakua na kuonekana katika uhalisia wake: iwe ni ya matunda, kupata kivuli, yenye sifa za dawa, kupata mbao/nguzo/kuni au kuhifadhi udongo na mazingira.

### SHERIA ZIFUATWE KIKAMILIFU

Pili, juhudi zifanyike ili sheria/kanuni zilizopo zitekelezwe kuanzia Serikali za Vijiji, Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu na Taasisi husika pia kushirikiana na Sekta binafsi: iwe kwenye shule za msingi, sekondari na hata vyuo vya kati na juu. Iwapo sheria/kanuni zake zilizopo hazitoshelezi kwa maana ya kutokuwa na nguvu au kutotekelezeka ipasavyo; marekebisho yafanyike haraka.

### TULINDE VYANZO, KINGO ZA MITO

Tatu, vijito na mito, vyanzo vyake vilindwe (hasa misitulindimaji) na maeneo mengine muhimu kama ardhioevu. Kadhalika, kuhakikisha uotoasili unarejea kwenye ukanda wa mita 30/60 (safeguard-zone) kutoka kingo za vijito/mito pande zote mbili kulingana na ukubwa wa kijito/mto.

Hali hiyo iwe tangu mto unapoanzia hadi mwisho wake mfano, kuanzia Mto Ruaha Mkuu na vijito vinavyoingiza maji tuhakikishe uhifadhi wa kingo unarejea. Mto Rufiji na mingineyo yote inayoingiza maji baharini ilindwe ipasavyo.

Kilimo cha aina yoyote kifanyike nje ya ukanda wa mita 60 toka ukingo wa mto kwa mito mikubwa na vijito/mito midogo mita 30 ili kuondoa athari za mito kujaa udongo, mchanga na takangumu.

Bila kufanya hivyo, tutajikuta baada ya miaka kadhaa Bwawa la Mwalimu Nyerere litaonekana lina maji kumbe kina cha kuhifadhi maji kimepungua kutokana na kujaa udongo/mchanga (siltation).

Hali hiyo, ikiendelea kutokea taifa litapata hasara kubwa kwa kukosa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu kwa sababu maji kupungua haraka. Uhifadhi imara unatakiwa pia kwa mabwawa ya Mtera, Kidatu, Kihansi, Nyumba ya Mungu, na kwenye Mto Kagera (Rusumo) ili kulinda uhai wa mabwawa hayo.

### TUCHAGUE VIONGOZI WALINZI WA MAZINGIRA

Nne, kwenye kaya zetu na sehemu za kazi, usafi wa mazingira utamalaki na kila mhusika awajibike ipasavyo. Katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa watakaochaguliwa wawe ni watu wa kuwajibika ipasavyo. Wasiwe ni watu wa kuona mambo yanaharibika bila kutochukua hatua stahiki.

Watendaji Kata wachakarike na magari ya kusomba taka ngumu yaonekane yakifanya kazi ipasavyo siyo tu katikati ya majiji, manispaa na miji bali hata sehemu zilizo nje ya hapo.

### TUFANYE TAFITI

Tano, wataalamu wa sekta husika wafanye utafiti wa kina kujua mpaka sasa mabwawa yameathiriwa kwa kiasi gani kutokana na kujaa udongo/mchanga na takataka nyinginezo na hatimaye waishauri serikali hatua za kuchukua kurejesha uhai wa mabwawa husika. Msisitizo wangu ni kuzisimamia sheria na kanuni zinazohusika kutunza misitu/mazingira na vyombo husika visilaze damu wakati wa kulisaidia taifa na watu wake ni sasa.

**Tusilegeze kamba bali juhudi zipate msukumo toshelezi kiasi kwamba miti ikioteshwa inatunzwa, inakua na kuonekana katika uhalisia wake: iwe ni ya matunda, kupata kivuli, yenye sifa za dawa, kupata mbao/nguzo/kuni au kuhifadhi udongo na mazingira.**

Kimsingi hatujui kesho mambo yatakuwaje ingawa tunatakiwa kuweka mipango sahihi inayotekelezeka. Wizara za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Makamu wa Rais-(Mazingira) na Wizara ya Maliasili na Utalii zishirikiane vya kutosha kuhakikisha mazingira yanalindwa ipasavyo.

Hii ni pamoja na wizara zinazohusika na ardhi, nishati, kilimo, mifugo na uvuvi, afya, madini, viwanda na biashara pamoja na uwekezaji na vyombo vyake waweke mbele kila wakati ajenda ya mazingira na kushirikiana kwa hali ya juu.

### NEMC ONGEZENI MAKALI

Baraza la Taifa la Kusimamia Mazingira (NEMC) wasimamie utekelezaji wa sheria na kanuni ipasavyo bila kufumbia macho wala kumwonea mtu.

Kuwepo na wepesi wa kuchukua hatua kabla hali haijawa mbaya na wahusika kuwajibika ipasavyo. Suala la kulinda mazingira ni la kufa na Kupona hivyo NEMC wanatakiwa kutimiza wajibu na sio kufanya kazi kwa mazoea jambo ambalo halifai kabisa bali 'vaeni silaha viunoni mwenu mkalipiganie taifa' ipasavyo.

Naamini kila mdau akitimiza wajibu wake ndani ya miaka michache ijayo, tutaweza kuyashuhudia mabadiliko tarajiwa.

Mungu ibariki Tanzania

# Kampeni zaanza kwa kifo cha mmoja na kadhaa kujeruhiwa

**KIGALI, Rwanda**

MTU mmoja amefariki dunia na wengine kadhaa kujeruhiwa wakati wa mvutano kwenye mkutano wa kampeni za uchaguzi wa Rais wa Rwanda, Paul Kagame, maafisa wamesema.

Kampeni za uchaguzi mkuu wa Julai mosi zilianza Jumamosi, huku Rais Kagame akifanya mikutano miwili kaskazini mwa Rwanda mwishoni mwa wiki.

Ajali hiyo ilitokea Jumapili wilayani Rubavu, ambapo watu 37 walijeruhiwa, wanne kati yao wamelazwa hospitalini wakiwa na majeraha mabaya, taarifa ya Wizara ya Serikali za Mitaa ilisema.

Iliomba msamaha kwa familia ya marehemu na kuongeza kuwa timu ya matibabu kwenye eneo la mkasa ilifanya kila linalowezekana.

Rais Kagame (66), anawania muhula wa nne. Amekuwa Kiongozi Mkuu wa nchi hiyo tangu mwaka 1994, wakati kundi lake la waasi la wakati huo, Rwanda Patriotic Front, lilipotwaa mamlaka mwishoni mwa mauaji ya kimbari yaliyoelekezwa kwa watu wa kabila lake la Watutsi.

Alishinda uchaguzi uliopita wa urais mwaka 2017 kwa karibu asilimia 99 ya kura.

Rais Kagame na chama chake cha RPF Inkotanyi, hawajatoa maoni yao kuhusiana na kifo hicho.

Hata hivyo, Jumatatu asubuhi, RPF Inotanyi ilichapisha video kwenye Facebook ya Rais Kagame akipanda jukwaani kwenye mkutano huo uliohudhuriwa na takriban watu 250,000. BBC.

# Ruto awaaga polisi 400 wanaokwenda Haiti

**NAIROBI, Kenya**

RAIS wa Kenya, William Ruto, amewaaga maafisa 400 wa polisi wanaotarajiwa kuongoza ujumbe unaoungwa mkono na Umoja wa Mataifa (UN) kukabiliana na ghasia za magenge nchini Haiti, afisa wa serikali na chanzo cha polisi kimesema.

Taifa hilo la Afrika Mashariki lilijitolea kutuma polisi 1,000 ili kuleta utulivu nchini Haiti, pamoja na vikosi kutoka nchi nyingine kadhaa, lakini kupelekwa kwao kumekumbwa na matatizo ya kisheria.

Hata hivyo, Rais Ruto amekuwa akiunga mkono misheni hiyo kwa shauku na maafisa walisema mwishoni mwa wiki kwamba kikosi kingeondoka jana Jumanne.

Kutumwa huko kuliidhinishwa na Azimio la Baraza la Usalama la UN Oktoba, mwaka jana na kucheleweshwa na uamuzi wa Mahakama ya Kenya Januari, mwaka huu.

Mahakama ilisema utawala wa Rais Ruto hauna mamlaka ya kutuma maafisa nje ya nchi bila makubaliano ya awali ya nchi mbili.

Wakati serikali ilipata makubaliano hayo na Haiti Machi, mwaka huu, chama kidogo cha upinzani kiliwasilisha kesi mpya katika jaribio jingine la kuyazuia.

Nchi nyingine ambazo zimeonyesha nia ya kujiunga na misheni hiyo ni pamoja na Benin, Bahamas, Bangladesh, Barbados na Chad. BBC.





# Watu 22 wafa kiwanda kikiwaka moto

**SEOUL, Korea Kusini**

MOTO mkubwa wa kiwanda ulioanza baada ya betri kadhaa za lithiamu kulipuka umeua takriban watu 22 nchini Korea Kusini.

Moto huo ulizuka Jumatatu asubuhi kwenye kiwanda cha Aricell katika mji wa Hwaseong, takriban kilomita 45 kusini mwa Mji Mkuu Seoul.

Picha za runinga za ndani zilionyesha moshi mkubwa na milipuko midogo ikitokea wakati wazima moto wakipambana kuzima moto huo. Sehemu ya paa ilikuwa imeanguka.

Korea Kusini ni mzalishaji mkuu wa betri za lithiamu, ambazo hutumiwa katika vitu vingi kutoka kwa magari ya umeme hadi vikapatilishi bebe.

Afisa wa zima moto, Kim Jin-young, alisema Wachina 18, raia mmoja wa Laos na wafanyikazi wawili wa Korea Kusini, wamethibitishwa kuwa miongoni mwa waliofariki dunia.

# UN: Sudan yaongoza kwa wingi wa watoto waliokimbia makazi duniani

**KHARTOUM, Sudan**

MKUU wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Catherine Russell, amesema Sudan ina idadi kubwa zaidi ya watoto waliokimbia makazi yao duniani.

Russell pia alionya kuwa mamilioni ya watoto wa Sudan, wana utapiamlo na karibu wote wameacha shule.

Russell anasafiri kuelekea Sudan huku ilani ya njaa ikizidi kuongezeka.

"Watoto wako kwenye hatari kubwa ya janga hili la njaa, alisema: milioni tisa hawapati chakula cha kutosha mara kwa mara, karibu milioni nne wanakabiliwa na utapiamlo mkali," alisema na kuongeza:

"Pia kuna shida ya kusoma, karibu watoto wote wa nchi hawako shuleni, katika hatari ya kuwa kizazi kilichopotea ambacho kinaweza kuchangia kukosekana kwa utulivu siku zijazo."

Licha ya hali mbaya ya kibinadamu, juhudi za Marekani za kuanzisha upya mazungumzo ya amani zimeshindwa.

Na matakwa ya Umoja wa Mataifa ya kusitisha mapigano katika mojawapo ya maeneo makuu ya vita, mji unaozingirwa wa El Fasher, yamepuuzwa. BBC.



# Umri wagubika mdahalo wa kwanza wa Biden,Trump

**NAIROBI, Kenya**


JOE Biden na Donald Trump, wagombea wawili wakongwe zaidi kuwahi kugombea urais wa Marekani, umri ni suala la uchaguzi na wala hawawezi kulikwepa.


Alhamisi iliyopita, Rais wa sasa wa chama cha Democratic, Biden (81) na mtangulizi wake wa chama cha Republican, Trump (78), watachuana huko Atlanta, Georgia, kwa mdahalo wa kwanza kati ya miwili kabla ya uchaguzi wa Novemba, mwaka huu.

Kwa dakika 90, Rais Biden na Rais wa zamani Trump, watazungumza juu ya masuala kdhaha ikiwa ni pamoja na uchumi na vita vya kigeni hadi uhamiaji na mustakabali wa demokrasia.

Kuteleza, kujikwaa au kupotosha kwa maneno, kunaweza kuzidisha wasiwasi kuhusu umri wao mkubwa, kukiwa na uwezekano wa kuunda upya kinyang'anyiro cha urais ambacho tayari kilikuwa kigumu wakati wapiga kura wanaanza kuwa makini.

Lakini kutoa utendaji mzuri, kunaweza kuwa muhimu zaidi kwa Rais Biden, Rais mkongwe zaidi wa taifa hilo ambaye amekuwa akikabiliwa na maswali kuhusu uwezo wake na utimamu wake wa kiakili tangu aingie madarakani.





"Hakuna kuficha ukweli kwamba Biden mwenye umri wa miaka 81, hakuna kuficha ukweli kwamba Trump kimsingi, ana umri sawa," alisema Jim Messina, mwanamkakati wa Kidemokrasia ambaye alisimamia kampeni "Siyo mashindano ya umri, ni mashindano ya sera na tabia. Sehemu ya kile kinachohitajika kutokea kesho usiku ni kuanza tu mazungumzo kuhusu tofauti kati yao," alisema Messina.

Sudan sasa ina idadi kubwa ya watoto walioachwa bila makao kote duniani ya urais ya Barack Obama 2012. BBC.

# Maquiz; Bendi iliyotikisa 'viota' vya burudani-2


Tshimanga Kalala Assosa


Dekula Kahanga 'Vumbi'

**Wiki iliyopita kuwaletea sehemu ya kwanza ya historia ya Maquiz, wiki hii Mwandishi Wetu Hamid Yassin kwa msaada wa vyanzo mbalimbali, anakuletea sehemu ya pili ya makala hiyo ya Maquis du Zaire iliyotamba vilivyo hapa Tanzania kuanzia miaka ya 1970 hadi 1990.**

MAQUIS du Zaire ambayo ilikuwa ikipiga muziki mara moja kwa wiki, ilikuwa ikifika usiku wa manane, wanasitisha muziki na kusikika kipaza sauti kikiuliza kama wapenzi wao walikwenda ukumbini na miswaki?

Wapenzi walikuwa wakijibu ndiyooooo… Wanaelezwa dawa ya meno ipo hapo. Muziki ulikuwa unapigwa hadi alfajiri.

Bendi hiyo ikiwa hapa nchini ilikuwa ikipiga na kucheza katika mitindo mbalimbali kwa nyakati tofauti. Mitindo hiyo ilikuwa ya Chakula Kapombe, Kamanyola, Bishe Bishe, Zembwela, Chekecha na Ogelea Piga mbizi.

Mwema Mudjanga 'Mzee Chekecha' ndiye aliyekuwa akinogesha zaidi mitindo hiyo. Alikuwa kivutio kikubwa ukumbini licha ya kazi yake ya kupuliza tarumbeta, alikuwa 'rapa' aliyeweza kuwainua vitini wapenzi kwenda kucheza, akitumia vibwagizo vya 'Chekeee…. Chekechaaa' 'Tusangalaa', 'aima imaa', 'Bishe bishee', 'cheza Kamanyolaa', 'cheza kwa maringo', ' Cheza ukijidai' ' Sanifuu Saa… Sanifu, Ongeleaa piga mbizi … na mengine mengi.

Maquis du Zaire wakati huo ilikuwa imesheheni wanamuziki zaidi ya 40 wenye vipaji vinavyopishana. Kwa idadi hiyo, laiti kama wangelikuwa na tamaa, wangeliweza kupiga muziki katika kumbi tatu tofauti kwa wakati mmoja.

Nina uhakika kwamba msomaji wangu una shauku ya kujua au kukumbushwa kikosi kamili kilichokuwa kinatengeneza Maquis du Zaire wakati huo.

Nikianza na safu ya waimbaji walikuwepo akina Mbuya Makonga 'Adios', Mutombo Lufungula 'Audax', Mukumbule Lolembo 'Parashi', Kabeya Badu, Kalala Mbwebwe, mapacha Kassalo Kyanga na Kyanga Songa.

Wengine walikuwa Kiniki Kieto, Abubakar Kasongo Mpinda 'Clayton', Mbombo wa Mbomboka, Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki', Tshimanga Kalala Assosa, Kabeya Badu, Masiya Radi 'Dikuba kuba', Issa Nundu na Tabia Mwanjelwa, Rahma Shaari na Anna Mwaole.

Wapiga gita la solo alikuwepo Chimbwiza Nguza Mbangu 'Nguza Vicking' ambaye kwa umahiri wake wa kulicharaza gita hilo, wapenzi walimpachika cheo cha juu kabisa jeshini cha 'Field Marshal'.

Wengine katika gitaa hilo walikuwa akina Ilunga Lubaba, Dekula Kahanga 'Vumbi' na Mbwana Suleiman 'Mbwana Cox'.

Gitaa la rhythm walikuwepo Mulenga Kalonji 'Vata', Omari Makuka na Steven Kaingilila Mauffi. Bila kuwashau akina Mbambu Kazadi, Mondo Mondonde na Nawayi Kabwila.

Gitaa zito la besi lilikuwa likiungurumishwa na Ilunga Banza 'Banza Mchafu' ambaye alijizolea umaarufu mkubwa kwa kulicharaza gita hilo akiwa kajitwisha kwenye upara kichwani kwake. Wengine walikuwa Ibrahimu na Mujos wa Bayeke.

Kama nilivyokujuza hapo awali kwamba bendi hiyo ilikuwa imejaza mseto wa vipaji mbalimbali. Kwa upande wa wapuliza Saxophone 'mdomo wa bata' walikuwepo akina Mafumu Bilali 'Bombenga 'Super Sax', Khatibu Iteyi Iteyi, Alex Kanyimbo, Kalamazoo, Akulyake Suleimani 'King Mallu', Roy Mukuna 'Mukuna wa Mukuna', Chibangu Katayi , Comson Mkomwa na Majengo Selemani.

Wapuliza tarumbeta walikuwepo akina Mwema Mudjanga 'Mzee Chekecha' Nkashama Kanku Kelly, Mioma wa Mwamba 'Mzee Tito', Kayembe Ndalabuu 'Trumbloo' Mpoyo Kalenga, Berry Kankonde, Kaumba Kalemba, Ngoi Mubenga, Ilunga Ngoi 'Bizos', Morgan Machege na Ngenda Kalonga.

Vijana hao kwa pamoja walikuwa wakitoa burudani maridadi wakiwa wamejitwisha tarumbeta zao vichwani wakilishambulia jukwaa, huku wakicheza kwa staili za aina yake ukumbini.

Madoido na mbwembwe hizo, ziliwavutia wapenzi wengi na kupenda kuhamisha viti vyao wakisogea sehemu iliyokuwa karibu, ili kushuhudia vijana hao wakifanya maajabu ya kuchezea vyombo hivyo.


Skasy Kasambula akiwa na mapacha Kassalo Kyanga na Kyanga Songa

Mbonyezaji wa Kinada alikuwa Mbuya Makonga 'Adios' huku Mutombo Sozzy akizicharaza drums akisaidiana na Matei Joseph. Tumba zilikuwa zikigongwa na Siddy Morris 'Super Konga' na Pulukulu Wabandoki Motto.

Walikuwepo na wanenguaji mahiri ambao walikuwa wakitoa burudani za pekee wakati huo akina 'Washa Washa', Dulla 'Panga Panga', Wandema Rashidi, Anna Mganga, Kinacho, Mwajuma, Frida Shirima, Zuwena na Ngalula Tshiandanda, wakiongozwa na Nkulu Wabangoi.

Ikiwa White House bendi hiyo ilitoka na vibao vingi vikiwemo vya Double double, Clara, Kyembe, Maiga, Mpenzi Luta, Mwana yoka ya Babote, Ngalula, Nasononeka, Nimepigwa ngwala, Promotion, Ngalula, Karubandika na Noelle Bonane wimbo ambao ulikuwa ukipigwa mahsusi nyakati za Krimasi na mwaka mpya.

Zingine zilikuwa Dora mtoto wa Dodoma, Balimwacha, Malokelee, Promotion, Seya, Sophia, Sumu ya mapenzi, Sababu ya nini, Zowa, Uba, Safari ya Mbeya, Wakati nikiwa mdogo na nyingine nyingi zisizo idadi.

Kuna msemo usemao "Cha kuazima hakistiri maungo" msemo huo uliisibu bendi ya Maquis du Zaire baada ya kuingia katika maelewano 'hafifu' na mwenye ukumbi, hadi kulazimika kuondoka wakiacha ukumbi huo ukibadilishwa kuwa Gereji hadi leo.

Baadaye bendi hiyo ikabadilishwa jina na kuwa Maquis Original wakipiga katika kumbi za Wapiwapi's pale maduka mawili, Chang'ombe na CCM Kata ya 14 Temeke, kabla ya kuhamia ukumbi mpya kwa wakati huo wa Lang'ata pale Kinondoni.

Maquis Original ilileta wanamuziki wengine toka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo muda mfupi kabla ya mpiga gitaa la solo, Dekula Kahanga 'Vumbi' kuondoka kwenda Stockholm nchini Sweden.

Wanamuziki hao walikuwa Kivugutu Motona Chatcho (Solo), na waimbaji Freditto Butamu na Luhembwe Mwahitwa 'Bobo Sukari'.

Walitikisa ukumbi wa Lang'ata kwa nyimbo zao kali za Mangolibo, Mayanga, Kisebengo, Makumbele, zikisindikizwa na wimbo wa Ngalula ambao mwimbaji Thsimanga Kalala Assosa alikuwa akitoa kibwagizo wakati wa 'chorus' akiita "Vumbiii Vumbiii Vumbiii. Nyimbo zote zilipigwa na kutamba kwa mitindo ya 'Washawasha' na 'Sendema'.

Maquis Original ikiwa Lang'ata, kuna shabiki mmoja aliyejulikana kwa jina la 'Magoma moto' ambaye alikuwa kivutio kikubwa kwa wapenzi wa Maquis, kwa kuonyesha uhodari wa kucheza 'Sendema' akiwa kajitwisha chupa ya Bia juu ya kichwa chake.

Ikumbukwe kwamba idadi kubwa mno miongoni mwa wanamuziki wanaotajwa humu, wameshatangulia mbele za haki.

Mungu aziweke roho zao pahala pema peponi waliotangulia. Amina.

# Arteta; Utoto, kazi na familia

**LONDON, England**

TUMEMWONA kama mchezaji na tunamfahamu kama meneja, lakini Mikel Arteta ni nani hasa?

Katika wiki ya mwisho ya msimu wa kusisimua wa Ligi Kuu ya Uingereza, meneja wa Arsenal alimualika mwandishi wa BBC Sport Guillem Balague nyumbani kwake kwa mahojiano ya kipekee ya saa moja.

Arteta amezungumza juu ya utoto wake, kazi yake, maisha yake ya familia na Umeneja wake kazi anayoifanya sasa.

### MAISHA YA UTOTONI YA ARTETA NA LA MASIA

Arteta alikulia katika kitongoji kizuri cha Antiguo huko San Sebastian.

"Ninapenda maji, napenda jua na napenda ufuo, na jumuisha mpira wa miguu juu ya hayo," anasema.

"Hapo ndipo nilitumia saa nyingi za mchana, nikicheza ufukweni nilipokuwa mtoto. Kwangu mimi, ilikuwa mchanganyiko mzuri."

Akiwa na umri wa miaka 14, Arteta alikutana na kipa wa baadaye wa Uhispania na Liverpool Pepe Reina katika siku yake ya kwanza katika Chuo cha mafunzo ya soka cha Barcelona, La Masia. Alikuwa rafiki na kulala chumba kimoja na magwiji wa Barca, Victor Valdez na Andres Iniesta wakiwa vijana.

"Yeye (Reina) amekuwa mmoja wa marafiki zangu wa karibu," asema. "Tulishiriki vitanda vyetu kwa miaka mitatu. Mojawapo ya kumbukumbu nzuri zaidi ambayo ninayo maishani mwangu ni wakati tuliotumia pamoja.

"Tulikuwa tukishindana kwa sababu ilitubidi, kwa sababu sote tulitaka kufika kwenye kikosi cha kwanza - lakini ilikuwa hisia halisi ya familia."

### ARTETA KUHUSU PSG 'MLINZI' POCHETTINO

"Mauricio alikuwa kama ngao kwangu, alikuwa akinilinda dhidi ya kila kitu. Alinipa imani na kujiamini sana," Arteta anasema.

"Alikuwa akicheza nyuma yangu na ilikuwa kama kuwa na mtu anayekusukuma mgongoni mwako na kukufundisha na kukusaidia kila wakati. Sikuweza kupata mtu yeyote bora zaid yake."

Kuhusu kuhamia PSG, Arteta anasema; "Ulikuwa uamuzi mgumu. Ndoto yangu ilikuwa kuichezea Barcelona lakini wakati huo ilibidi nifuate uhalisia wa mambo."

### 'KUISHI AU KUFA' KWA ARTETA HUKO RANGERS.

Mnamo 2002 Arteta alisaini mkataba wa kujiunga na Rangers, alipoondoka Barcelona.

"Sijawahi kuona hali kama hii, kuangalia jinsi watu hawa wanavyoipenda soka," anasema Arteta kuhusu ziara yake ya kwanza katika Rangers, ambapo walikuwa wakicheza na PSG katika Ligi ya Mabingwa.

"Uamuzi bora zaidi tuliofanya. Ilikuwa ngumu sana, soka tofauti kabisa. Lazima uishi au ufe."

Wakati akiwa Rangers, Arteta alikutana na mwanamke ambaye alikuwa mke wake baadaye, Bi Lorena, mkufunzi wa masuala ya maisha, kwenye safari ya kwenda San Sebastian. Sasa wana watoto watatu pamoja.

"Amebadilisha maisha yangu. Amebadilisha mtazamo wangu kuhusu maisha," anasema.

"Tumepitia hali nyingi, nyingi tofauti, zingine za kuvutia, zingine ngumu sana.

Nina hisia na yeye kwamba hatuwezi kuchokana. Ninaweza kukaa hapo saa tano, saa 10, kwenda popote duniani na kufurahia na kufurahi na kucheka."

Anasema katika taaluma yao huwa wanazungumza kuhusu mhusika mkuu ambaye ni mchezaji au kocha au meneja, lakini anauliza vipi kuhusu mtu ambaye yuko karibu na huyo? Na bila huyo hakuna misingi ya kutosha na hakuna nguvu za kutosha za kuwa thabiti.

### HISIA ZA HUZUNI JUU YA TALAKA YA WAZAZI WA ARTETA

Baada ya kuishi Uskochi, Arteta mwenye umri wa miaka 24 alihamia Real Sociedad ya Uhispania kwa matumaini ya kuweka familia yake pamoja baada ya wazazi wake kusema walikuwa wakitalikiana.

"Nilijihisi kuwa na huzunni na hatia. Sikujua kama hiyo ilikuwa ni kwa sababu yangu na kujaribu kutekeleza ndoto yangu. Ninahisi kuwajibika sana kwa hilo," anasema.

"Sikuwahi kuhisi kuwa ulikuwa wito sahihi [kurejea Uhispania], lakini nilikuwa na jukumu na nilitaka kuwaunganisha tena wazazi wangu na familia yangu.

"Ilikuwa balaa. Haijawahi kufanya kazi kwa maana hiyo. Sijawahi kuhisi kuunganishwa kwa wakati wowote."



### ARTETA JUU YA 'KUPENDA KILA DAKIKA' HUKO EVERTON

Arteta alijiunga na Everton mwaka wa 2005 kwa pauni milioni 2 baada ya kufanikiwa kupata mkataba wa mkopo kutoka Sociedad.

"Moja kwa moja, unaungana na timu, unaungana na wachezaji, unaungana na wafanyakazi, unaungana na wafuasi. Na hisia hiyo inahitajika," anasema.

"Unajiamini, unajisikia

Arteta juu ya 'kupenda kila dakika' huko Everton Arteta alijiunga na Everton mwaka wa 2005 kwa pauni milioni 2 baada ya kufanikiwa kupata mkataba wa mkopo kutoka Sociedad.

"Moja kwa moja, unaungana na timu, unaungana na wachezaji, unaungana na wafanyakazi, unaungana na wafuasi. Na hisia hiyo inahitajika," anasema.

"Unajiamini, unajisikia msisimko kila asubuhi kushuka kitandani na kwenda kwenye mazoezi. Nilipenda kila dakika."

### ARTETA KWENYE 'UELEWANO WA AJABU' AKIWA NA GUARDIOLA

Muda mfupi baada ya maisha yake ya uchezaji kuisha, Arteta aliyekuwa na umri wa miaka 34 alijiunga na Manchester City kama meneja msaidizi wa Pep Guardiola.

### "TULIKUWA NA UELEWANO MZURI WA AJABU," ANASEMA.

"Kwa kutazamana kwa macho tu tulielewana wazi juu ya kile tulichopaswa kukifanya au kile tulichokuwa tunafikiria wakati huo.

Anaongeza kuwa, lilikuwa ni jambo la kuvutia kuwa sehemu ya kitu kipya.

### ARTETA NA ARSENAL YA WAKATI HUO NA SASA

Arteta aliichezea Arsenal kati ya 2011 na 2016. Alipojiunga mara ya kwanza, alikuwa akiongea kwenye chumba tulivu cha kubadilisha.

Anasema; "Nilianza kuzungumza na nikaanza kuwaunganisha watu wote; 'Njoo, tufanye hivi, nyie'. Nilisisimka sana.

"Nitafanya kila kitu. Nitavunja kila ukuta hapa. Tunapaswa kufanya hili kutokea.", anakumbuka.

Anaongea nini juu ya kuhusu kustaafu; "Ilikuwa inafikia hatua ambayo nilikuwa nahisi kupendezwa zaidi na upande wa kufundisha kuliko upande wa kucheza."

### DESEMBA 2019 ARTETA ALIKUA MENEJA WA ARSENAL

"Suala lilikuwa la kina zaidi. Suala lilikuwa kwenye mizizi yetu. Yote yalikuwa ni fujo," anasema.

"Tunahitaji watu wetu. Tunahitaji kuwashawishi kwamba umejitolea na uko tayari kuipeleka klabu hii sehemu tofauti kabisa."

Arteta alipanda mzaituni mbele ya ofisi yake, kuashiria umri na mizizi ya klabu.

Anasema hivi; "Niliupanda mti huo na kusema, 'Hii ni zawadi yangu. Sasa unapaswa kuuangalia. Ni kitu kilicho hai. Huwezi kuuacha ife.'

"Mti huo ni kiasi sawa cha miaka katika klabu yetu ya soka, zaidi ya miaka 130.

"Utakuwa huko kila siku. Lazima muuangalie na nyote muwajibike."





Minong'ono ya usajili

# Dili la Chama lazidi kuzua kizungumkuti




USAJILI wa kiungo mshambuliaji Mzambia Clatous Chota Chama unazidi kuzua sitofahamu baina ya vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga.

Chama ana uwezekano mdogo kubaki Simba SC baada ya kudaiwa kuwa, amemalizana na Yanga.

Imeelezwa kuwa, usajili wake ndani ya Yanga umewahusisha wanachama wenye ushawishi na majina makubwa wa klabu hiyo, kama ambavyo walishiriki kwenye kumbakisha Aziz Ki Jangwani. MO Dewji anahitaji mchezaji mwingine kijana mwenye nguvu, Simba wanaamini pesa anazohitaji Clatous Chama wanaweza wakampata mchezaji mwingine mwenye uwezo na mwenye umri mdogo ambaye atakaa Simba kwa muda mrefu.

Habari zote na Valensi Mbaga

## Singida Black Stars washusha chuma kingine



KLABU ya Singida Black Stars imekamilisha usajili wa kiungo wa FC Lupopo, Mick Harvy Itali Ossété (24)

Usajili huo umefikiwa baada ya mazungumzo ya muda mrefu na uongozi wa mchezaji huyo. Kila kitu kimekamilika na kiungo huyo ni mali ya Singida Black stars.

## Simba yakaa mezani kumpata Okejepha



SIMBA SC na Rivers United wako kwenye hatua ya mwisho ya mazungumzo ya kumsajili beki wa Nigeria Augustine Okejepha kuhamia Tanzania.

Klabu hiyo imependekeza mkataba wa zaidi ya dola 100,000, pamoja na sehemu ya 40% ya ada yoyote ya uhamisho ya baadaye ikiwa atauzwa.

## Chikamso anukia Yanga



BEKI wa Enyimba Chikamso Okechukwu amejaa kwenye rada za Yanga SC na muda wowote kuanzia sasa watakaa mezani kwa ajili ya kuongelea dili hilo.

Yanga wanaweza kuanza kujadiliana na beki huyo mapema wiki hii ikiwa wanahitaji kuongeza nguvu kwenye eneo lao la kujilinda zaidi na kutengeneza kikosi imara.

## APR yamvalia njuga Skudu



KLABU ya soka ya APR ya nchini Rwanda imeanza mazungumzo rasmi na winga machachari wa Yanga SC Skudu Makudubela.

APR wameonyesha nia ya dhati kuhakikisha wanakamilisha usajili wa winga huyo.

## Inonga rasmi kukipiga AS Far Rabat



BAADA ya Simba SC kutangaza kutoendelea na beki Henock Inonga ambaye imekuwa naye kwa miaka mitatu tangu 2021, rasmi sasa Mkongomani huyo atakuwa sehemu ya kikosi cha AS Far Rabat ya Morocco kwa msimu ujao.

Mashabiki wa AS Far Rabat tayari wameshajiandaa kumpokea beki huyo japo bado dili lake halijajulikana kuwa la muda gani.

# Kona ya Urembo



# Mbinu mwafaka za kununua mavazi ya harusi







**Na Valensi Mbaga**

LAZIMA tuseme kuhusu mavazi ya harusi kwani kila mtu anayehudhuria harusi ana nia ya kuona mavazi ya bibi harusi. Kwa hivyo, ikiwa unapanga harusi yako lazima uwe na vazi ambalo utajisikia mrembo na ambalo litavutia macho ya kila mtu. Je, unawezaje kununua mavazi ya harusi? zingatia sheria chache rahisi za kununua mavazi ya harusi kama ifuatavyo.

### 1. ANZA UTAFUTAJI WAKO MAPEMA

Utafutaji wa mavazi ya harusi unapaswa kufanyika kwa kasi ya utulivu ili usifanye uamuzi wa haraka na kuishia na mavazi ambayo hupendi. Mara tu tarehe itakapowekwa, anza kuangalia nguo popote unapoweza kuzipata. kwa mfano, Mtandao, ni chanzo bora cha msukumo kwa miundo ya mavazi ya harusi. Unaweza pia kufika kwenye maduka mazuri ya harusi kama yapo katika mji wa karibu na uangalie.

### 2. WEKA BAJETI

Baada ya kutazama kwenye maduka ya harusi na unajua ni kiasi gani cha nguo kitakugharimu, weka bajeti. Ongeza pesa kidogo juu ya vifaa, gharama za kusafisha na matengenezo ya dharura. Mara baada ya kuweka bajeti, unaweza kununua karibu na nia ya kupata mpango bora zaidi, kwa mavazi yaliyo tayari au mavazi yatakayotengenezwa.

### 3. FANYA UTAFITI WAKO

Wakati wa kununua mavazi ya harusi, kumbuka kuwa nguo hizo sio za kawaida. Kuna mitindo maalum ambayo inafaa maumbo fulani ya mwili. Kabla ya kuamua juu ya muundo, tambua sura ya mwili wako, na kisha uangalie mitindo inayofaa sura hiyo. Duka zuri la mitindo ya harusi au mshonaji anapaswa kuwa na uwezo wa kukupa ushauri sahihi juu ya aina ya mavazi ambayo ingefaa zaidi kwako.







### 4. SHIKILIA MAONO YAKO

Nguo unayochagua inapaswa kuendana na wazo lako la harusi. Kwa mfano, ikiwa unapanga harusi ya nje, muundo wa mavazi unapaswa kuwa vizuri kuvaa nje. Ikiwa unapanga harusi ya jioni ya jioni, mavazi inapaswa kuwa na mavazi ya chakula cha jioni au 'mavazi ya jioni. Pia, ikiwa unafanya harusi ya kitamaduni, mavazi yanapaswa kuonyesha utamaduni na uzuri wa hafla hiyo.

### 5. MSHIRIKISHE RAFIKI PAMOJA

Ni wazo zuri kuwa na rafiki anayeweka alama pamoja unapopita mjini kutafuta nguo za harusi. Rafiki huyu atakuwa kioo chako unapojaribu mavazi na atakupa maoni ya uaminifu wakati umekwama kwenye mavazi gani ya kuchukua. Rafiki mmoja au wawili tu wanatosha, ingawa, watu wengi wanaweza kuishia kukuchanganya!

### 6. BEBA VIFAA VYAKO

Je, mavazi utakayochagua yatalingana vipi na vifaa unavyokusudia kuvaa? Njia bora ya kujua jinsi kila kitu kinavyolingana ni kubeba pamoja unapoenda kutafuta vifaa. Vifaa ni pamoja na pete, mkufu, vikuku na vitu vingine vya kujitia. Waweke unapojaribu kwenye kila vazi ili uone athari kamili.

### 7. VIPI KUHUSU UHAKIKI?

Je, kitaalam ni muhimu wakati wa kununua mavazi ya harusi? Ndiyo wanafanya! Kwanza, unahitaji kujua nyenzo gani ni bora kwa mavazi. Pili, lazima ujue wabunifu bora na wauzaji wa harusi katika eneo lako ni nani. Tatu, unahitaji kuona jinsi nguo zilizofanywa na wabunifu hawa zinavyoonekana. Kwa maoni ya uaminifu juu ya nguo za harusi, angalia tovuti na kurasa za mitandao ya kijamii za wabunifu na maduka ya harusi unayopenda.

### 8. FANYA MAJARIBIO

Mara baada ya kuamua juu ya kubuni, chagua mavazi na ujaribu; si mara moja au mbili, lakini mara kadhaa! Ikiwa unununua nguo iliyopangwa tayari, itahitaji kurekebishwa, wakati nguo iliyopangwa itahitaji vipimo na 'fittings' kadhaa kabla ya kuwa kamilifu. Kumbuka kwamba jambo muhimu zaidi ni kufaa, si ukubwa wa mavazi. Kufaa kwako mwisho lazima iwe angalau wiki moja kabla ya harusi!

### 9. SAINI MKATABA

Mkataba na mtengenezaji wa mavazi yako ni muhimu. Makubaliano yaliyoandikwa yatahakikisha kwamba nyote wawili mtashikamana na makubaliano kuhusu ununuzi, marekebisho na utoaji wa mavazi. Ili kuepuka kukata tamaa katika dakika ya mwisho, andika kila kitu kwenye karatasi, na uombe risiti kwa kila malipo.

Vidokezo hapo juu vitakusaidia sana unapoanza mchakato wa kununua mavazi ya harusi. Jambo la mwisho unapaswa kuwa wewe mwenyewe katika mavazi, na inapaswa kutafakari utu wako halisi.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Juni 26 - Julai 2, 2024 |

# Mwamnyeto, Yanga hakijaeleweka



**Na Mwandishi Wetu**

NAHODHA wa Yanga, Bakari Nondo Mwamnyeto amemaliza mkataba wake na Wanajangwani hao, lakini bado wanavutana kusaini dili jipya.

Meneja wa mchezaji huyo, Carlos Sylivester 'Master Mind' amedai kuwa, wapo mezani na uongozi wa Yanga na mazungumzo yanaendelea vizuri.

Pia Carlos amepasha kuwa, mezani kwao wana ofa nono ya Simba kuliko ile ya Yanga na mchezaji wake yupo tayari kuichezea timu yoyote itakayomwaga dau kubwa kati ya hizo mbili.

# Fasika kumrithi Inonga Simba

## ●Mels apewa meno ya usajili Msimbazi
## ●Mzamiru apigwa 'pingu' hadi 2026



**Na Mwandishi Wetu**


WAWAKILISHI wa beki wa kati wa Cape town City, Raia wa Congo DR, Nathan Fasika (25) wanatarajia kutua nchini keshokutwa Ijumaa kufanya mazungumzo ya mwisho na Simba.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zimethibitisha kuwa, ni kweli wana nia ya kumsajili nyota huyo na sasa mbivu ama mbichi itajulikana Ijumaa hii ila Simba wana nia ya kuinasa saini ya beki huyo ili kuziba pengo la Inonga Backa.

Kwa sasa beki huyo anaitumikia klabu ya Vålerenga ya Norway kwa mkopo akitokea Cape town City ya Africa Kusini.

Wakati huo huo, Skauti Mkuu wa Simba, Mels Daalder kapewa nguvu yote katika kuijenga Simba upya kuelekea msimu ujao kinyume na hapo awali.

Kiongozi mmoja wa ngazi ya juu wa Simba amethibitisha kuwa, hivi sasa kila mchezaji anayependekezwa na yoyote basi lazima apitie kwa Mels kuchunguzwa na kujiridhisha.






"Mels atakwenda nchi anakotoka mchezaji husika ili kumjua vizuri kitabia na hata kuongea timu pinzani za ligi husika na mashabiki wake," amedai mtoa taarifa wetu.

Katika kuonyesha Simba wameamua na wako makini safari hii, Mels baada kukusanya taarifa na kujiridhisha ndipo atatoa uamuzi kama mchezaji husika asajiliwe au asisajiliwe. Huku bajeti yake ya kusafiri popote kufanya kazi zake imetengwa kabisa kuepuka visingizio.

Hii inaonyesha ule usajili wa kuambiwa tu na kutoa pesa umekwisha ndani ya Msimbazi hivi sasa Sayansi ya mpira imeanza kuchukua nafasi.

Katika hatua nyingine Klabu ya Simba imemuongezea mkataba kiungo wake mkabaji, Mzamiru Yassin wa miaka miwili kuendelea kusalia Msimbazi. Mkataba wa Mzamiru ulimalizika mwishoni mwa msimu huu na mapendekezo ya kiufundi yamependekeza mchezaji huyo kubaki kutokana na mchango wake, hivyo uongozi wa Simba imemuongezea miaka mingine miwili ya kuendelea kusalia kikosini.

# Italia nayo yatinga 16 Bora Ulaya

**LEIPZIG, Italia**

MABINGWA watetezi, italia wamefanikiwa kutinga hatua ya 16 Bora Kombe la Mataifa Ulaya 'Euro 2024' licha ya sare ya 1-1 na Croatia katika mchezo wa Kundi B usiku wa kuamkia jana Uwanja wa Leipzig Jijini Leipzig hapa nchini Ujerumani.

Kiungo mkongwe wa umri wa miaka 38, Luka Modri, wa Real Madrid alianza kuifungia Croatia dakika ya 55, dakika moja tu tangu mkwaju wake wa penalti uokolewe na kipa Gianluigi Donnarumma.

Lakini huku mashabiki wa Croatia wakifurahia na kuamini wamesonga mbele, kiungo wa Lazio, Mattia Zaccagni aliwainua mashabiki wa Italia na kuwanyamazisha wapinzani kwa kufunga bao la kusawazisha dakika ya nane na ya mwisho katika muda wa nyongeza baada ya kutimia dakika 90 za kawaida za mchezo.

Mechi nyingine ya Kundi B juzi bao pekee la mshambuliaji wa Barcelona, Ferran Torres García dakika ya 13 liliipa Hispania ushindi wa 1-0 dhidi ya Albania Uwanja wa Dusseldorf Arena Jijini Dusseldorf.



# Dk. Kikwete ataka soka la vijana litiwe mkazo

**Na Hellen Mwango**

RAIS Mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete amezishauri klabu za soka nchini kuwekeza kwenye timu za vijana sambamba na Serikali kufanya hivyo kwenye shule za msingi na sekondari ili kuibua vipaji vya kuendeleza mchezo huo.

Pia Rais huyo Mstaafu amelishauri Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Serikali, kupeleka walimu wa michezo kwenye shule mbalimbali ili kuibua vipaji na kuendeleza mpira wa soka unaopendwa na Watanzania wengi nchini.

JK alitoa kauli hiyo jana wakati akihojiwa na Kituo kimoja cha Redio jijini Dar es Salaam kuhusu Msoga Marathoni, ambapo alisisitiza kwamba, michezo iko mingi lakini Watanzania wanapenda sana mpira wa soka.



"Michezo ni mingi lakini Watanzania wanapenda sana mpira wa soka, mchezo ambao tunacheza tangu tukiwa wadogo tulianza na ile 'chandimu' tukitumia vitenesi mpaka mpira wa matambara yote hiyo imetujengea mapenzi japo mimi nikiwa Kibaha Sekondari nilikuwa mchezaji wa mpira wa kikapu (Basketi ball)," alisema Dk. Kikwete.

Alisema hali hiyo ndiyo imewajengea Watanzania kujua mpira wa miguu pekee tofauti na nchi nyingine ambako wanacheza michezo mingi tofauti.

Pia ameitaka serikali kukuza sekta ya michezo, kutengeneza mazingira mazuri kama wakati wake alipogharamia kuwaleta makocha wa michezo nchini ili kuiinua sekta hiyo kimataifa zaidi.

"Wakati wangu niliamua kuwalipia makocha wa michezo yote ikiwamo riadha, mpira wa pete na wa soka. Kwa sasa Serikali inajenga viwanja kwa ajili ya maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ni shindano kuu la soka la kimataifa katika bara la Afrika kwa hiyo tukiwa na timu za vijana zitaongeza zaidi thamini ya michezo nchini," alisema Dk. Kikwete.